COLGATE-PALMOLIVE COMPANY

# KANUNI YA MAADILI MEMA



# *Kuishi Kulingana na Maadili Yetu*

*KUJALI • KUFANYA KAZI PAMOJA DUNIANI • UBORESHAJI UNAOENDELEA*




*Kudumisha Viwango vya Juu zaidi vya Maadili*

# UJUMBE KUTOKA KWA MWENYEKITI WETU, RAIS NA CEO

Uongozi wa kimaadili umekuwa muhimu zaidi. Pamoja na maadili yetu ya Kujali, Kufanya Kazi Pamoja Duniani Kote na Uboreshaji Unaoendelea, sifa ya Kampuni yetu ya uadilifu na viwango vya juu vya kimaadili imekuwa chanzo cha nguvu na faida kwa ushindani. Sifa yetu ni muhimu sana kwa watu wa Colgate, kwa watumiaji na wateja wetu, kwa wawekezaji wetu na washirika wetu wa biashara.

Tangu ilipozinduliwa karibu miaka 30 iliyopita, Kanuni yetu ya Maadili Mema inatuongoza kwa seti ya kanuni ambazo zinaangazia maadili ya Colgate na viwango vilivyowekwa ambavyo vinaongoza tabia zetu za kimaadili. Kanuni hizi huhakikiwa, husasishwa na kutolewa upya mara kwa mara ili kuhakikisha uendeleaji wa umuhimu wake. Kama kampuni kuu inayofanya kazi katika nchi nyingi duniani, sisi wote ni lazima tuhakikishe kwamba tabia na maamuzi yetu yanaafikia dhana na maadili yetu kama ilivyoandikwa katika Kanuni zetu.

Kila mmoja wetu hutoa maamuzi kila siku ambayo yanaweza kuathiri hali za kibinafsi, kifedha, kijamii au kimaadili. Kama mwanachama wa familia ya Colgate, ni muhimu usome, uelewe na ufuate kabisa Kanuni zetu ili kuhakikisha kwamba tunatoa maamuzi yanayoongozwa na uwajibikaji wetu wa kibinafsi wa kutenda kwa uadilifu na kwa viwango vya juu zaidi vya kimaadili.

Watu wa Colgate wanatarajiwa kuonyesha tabia yenye msimamo wa kimaadili kupitia matendo na maneno yao. Hii inajumuisha "Kuongea" ili kupinga tabia ambazo zinapingana na Kanuni zetu, pamoja na sera nyingine za Colgate au sheria husika.

Watu wa Colgate hujivunia sana matokeo yetu ya kibiashara. Matokeo ni muhimu, lakini vile vile na njia ambayo tunafikia matokeo hayo. Nawashukuru mapema jinsi mnavyoendelea kujitolea kushiriki katika maadilli yetu pamoja na uongozi wenu wa maadili ambao ni muhimu katika kuendeleza mafanikio ya biashara yetu.



Ian Cook
Mwenyekiti, Rais na CEO

# KUISHI KULINGANA NA MAADILI YETU

Kwa kuishi kulingana na maadili yetu ya Colgate ya Kujali, Kazi ya pamoja Duniani na Uboreshaji Unaoendelea, tunaunda utamaduni ambao watu wanafanya kazi kama timu, wakifanya kazi pamoja kuwadia lengo moja. Thamani tatu kuu za Colgate ni sehemu ya kila kitu tunachokifanya.

## KUJALI

Kampuni inawajali watu: Watu wa Colgate, wateja, wenye hisa, watumiaji, watoa huduma na wenzi wa biashara. Colgate imejitolea kutenda kwa huruma, uadilifu, uaminifu na kwa kiwango cha juu kabisa cha maadili katika hali zote, kuwasikiliza wengine kwa heshima na kuthamini utofauti. Kampuni imejitolea pia kulinda mazingira duniani, kuboresha jamii ambazo watu wa Colgate wanaishi na kufanya kazi, na kuafikiana na sheria na masharti yote ya serikali.

## KAZI YA PAMOJA DUNIANI

Watu wote wa Colgate ni sehemu ya timu ya dunia, waliojitolea kufanya kazi pamoja nchini kote na ulimwenguni kote. Kampuni inaweza kufikia na kudumisha ukuaji wa faida kwa kushiriki tu kimawazo, teknolojia na vipaji.

## UBORESHAJI UNAOENDELEA

Colgate imejitolea kujiboresha kila siku katika kila kitu inachofanya, kibinafsi na kama timu. Kwa kuelewa vyema matarajio ya watumiaji na wateja na kuendelea kufanya kazi ili kuvumbua na kuboresha bidhaa, huduma na michakato, Colgate itakuwa bora kabisa. Katika soko la leo lenye ongezeko la ushindani, maadili ya Colgate ndio msingi wa ufanisi wa watu binafsi, timu na kampuni. Ni kwa kuwaheshimu watu wengine tu na kuishi kulingana na maadili ya Colgate ndio tunatumaini kufikia matokeo bora ya biashara.

# KUSIMAMIA KWA HESHIMA

*"Kusimamia kwa Heshima" ndiyo njia watu wa Colgate hutumia ili kuendeleza Maadili ya Kampuni.*

Kwa Kusimamia kwa Heshima, tunaunda mazingira ambapo watu wanahisi huru kutoa mapendekezo, kuchangia mawazo na kuchangia shirika.

Kusimamia kwa Heshima huunda mazingira ambapo watu wanawajali wengine na wanafanya kazi pamoja ili kufikia uwezo wao kamili.

Kanuni za Kusimamia kwa Heshima ni:

## WASILIANA

Elezea mawazo waziwazi na kwa urahisi; wasikilize wengine; unda mazingira ambapo watu wako sawa kusema mawazo yao; kuza mtiririko wa maelezo kwa wakati unaofaa na unaoendelea kutoka na kuelekea kwa wengine.

## TOA NA UTAFUTE MAONI

Wainue watu wote wa Colgate kwa kutoa na kutafuta maoni mema na maalum; toa mwelekeo na wasaidie watu kuzingatia kubaki imara; himiza mabadiliko mema na kuza kazi ya kipekee.

## THAMINI MICHANGO YA KIPEKEE

Thamini na utambue michango na kazi nzuri ya wengine; heshimu upekee wa kila mtu; wahusishe wengine wakati wa kufanya maamuzi na kuimarisha vipaumbele. Kuwathamini watu kwa utofauti wao ndio ufunguo wa kujenga na kudumisha ufanisi katika biashara sasa na katika mustakabali.

## KUZA KAZI YA PAMOJA

Jenga ahadi za malengo ya pamoja; tatua migogoro kwa njia nzuri.

## ONGOZA KWA MFANO

Kuwa mfano mzuri wa kutekeleza biashara kwa njia ya kimaadili, usimamizi bora, na kwa kuunda mazingira ya kikazi yanayopendeza na yaliyo na usawa.

# FAHARASA


Kuhusu Kanuni ya maadili Mema

Uhusiano wetu na Kila Mmoja 9

- Tunajitahidi kuwa na mahusiano ya kikazi mazuri
- Tunakuza mawasiliano ya uwazi na ukweli
- Tunathamini watu wa Colgate kama rasilimali yetu kubwa zaidi

Uhusiano wetu na Kampuni 12

- Tunaepuka mingongano ya maslahi
- Tunalinda siri za biashara na maelezo ya siri ya Kampuni
- Tunafuata sera za wanahabari na vyombo vya habari
- Tunatunza vitabu na rekodi sahihi za kifedha
- Tunalinda mali ya Colgate
- Tunatumia rasilimali za teknolojia ya habari na mitandao ya kijamii kwa uwajibikaji

Uhusiano wetu na Bodi ya Wakurugenzi 19

- Tuna Bodi ya Wakurugenzi ambayo iko huru, yenye ujuzi na inayohusisha watu mbalimbali
- Tunakuza mawasiliano ya moja kwa moja na wazi na Bodi
- Tunajitolea kuwa na uongozi bora zaidi wa Kampuni

Uhusiano wetu na Mashirika ya Biashara Mengine 20

- Tunafanya kazi na wagavi, wateja na wahusika wengine kwa uadilifu
- Hatutoi au kupokea zawadi zisizofaa
- Tunaheshimu siri za biashara na maelezo ya siri ya wengine

Uhusiano wetu na Watumiaji 22

- Tunaweka viwango vya juu zaidi kwa bidhaa zetu
- Tunawajibu wateja wetu
- Utangazaji wetu ni wa kweli na sahihi

Uhusiano wetu na Serikali na Sheria 24

- Tunatekeleza sheria zote husika
- Tunatekeleza sheria za ushindani
- Tunatekeleza sheria za usalama
- Tunatekeleza sheria dhidi ya kutoa hongo
- Tunatekeleza sheria za biashara za kimataifa
- Tunatekeleza sheria za faragha ya data na ulinzi wa data
- Tunatekeleza sheri za kuweka rekodi
- Hatutoi michango ya kisiasa

Uhusiano wetu na Jamii 31

- Tunahusika katika kuchangia na kujitolea katika jamii
- Tunashirikiana na serikali kuhusu matatizo yanayoathiri biashara yetu
- Tunapinga tabia za ajira zozote za kudhulumu na zisizo za utu
- Tunaonyesha kujitolea kwetu kwa haki za binadamu duniani kote

Uhusiano wetu na Manzingira 33

- Tumejitolea kwa uendelezaji na uwajibikaji wa kijamii
- Tunalinda na kutunza sayari yetu

Uhusiano wetu na Washikadau 34

- Tunazingatia uongozi mzuri wa kampuni ili kulinda thamani ya washikadau wetu
- Tunadumisha mipango thabiti ya ukaguzi ili kuongeza imani ya wawekezaji
- Tunawafahamisha washikadau kuhusu maendeleo ya Kampuni

Uwajibikaji wa Makubaliano 35

- Mawasiliano na ufichuzi ni muhimu
- Tuna Kitengo cha Ajira cha kampuni kukusaidia ikiwa unahitaji mwongozo
- “Tunaongea” ili kuripoti matatizo kwa watu wanaofaa
- Hatua za kinidhamu zinaweza kuchukuliwa
- Kanuni hizi zinahusu watu wote wa Colgate na shughuli za Kampuni

# KUHUSU KANUNI YA MAADILI MEMA

Kanuni Yetu ya Maadili Mema ya Colgate hutumika kama rasilimali muhimu ya kuhakikisha shughuli zetu za biashara za kila siku zinatekelezwa kwa uadilifu. Kanuni hizi zinaonyesha wazi kwa kila mmoja wetu kwamba njia ambayo tunatumia kufikia matokeo ya biashara yetu ni muhimu. Kanuni ya Maadili inatumika kwa watu wote wa Colgate, hii ni pamoja na wakurugenzi, maafisa, na wafanyakazi wote wa Kampuni na mashirika yake tanzu. Wachuuzi na wagavi pia wanastahili kufuata mahitaji haya, kwani kuafikiana na Kanuni ya Maadili Mema ya Colgate ya Wahusika wengine ni sharti la kufanya biashara na Colgate.

Kila mfanyakazi ana jukumu la kuonyesha uadilifu na uongozi kwa kuafikiana na kanuni, Mwongozo wa Kanuni za Biashara Duniani, sera za Kampuni na sheria zote husika. Kwa kujumuisha kabisa maadili na uadilifu katika mahusiano na utoaji wetu wa maamuzi ya kibiashara, tunaonyesha kujitolea kwa utamaduni ambao unakuza viwango vya juu zaidi vya kimaadili.

Ikiwa una maswali au masuala yoyote kuhusu kufafanua au kutekeleza Kanuni hizi au sera na taratibu zozote zinazohusiana na Colgate, unastahili kujadili hali hiyo na meneja wako, Kitengo cha Ajira, Shirika Kuu la Kisheria au Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji.

Ni sera na desturi ya Colgate kudumisha viwango vya juu zaidi vya kimaadili na kuunda eneo huru la kazi lisilokuwa na tabia isiyofaa au ya kinyume na sheria, ambayo watu wanahimizwa kushiriki hoja zao na Kampuni bila uwoga wa kulipizwa kisasi. Kwa hivyo, katika Colgate, hakuna hatua yoyote mbaya itakayochukuliwa dhidi ya mfanyakazi yeyote, mfanyakazi wa zamani, wakala au mhusika mwingine kwa sababu ya kulalamikia, kuripoti, au kuhusika au kusaidia katika uchunguzi wa shuku ukiukaji wa Kanuni ya Maadili Mema ya Kampuni, sera ya Kampuni au sheria husika, isipokuwa kama madai au maelezo yaliyotolewa yanakutwa kuwa ya uwongo au hayakutolewa kwa imani ya ukweli. Kwa umbali unaowezekana, Colgate itadumisha siri ya malalamiko yote. Madai yote ya ulipizaji kisasi yatachunguzwa, na kama inafaa, hatua ya kinidhamu itachukuliwa, ikiwa ni pamoja na kusitishwa kwa ajira.

Kanuni hizi zinapatikana mtandaoni na zimetafsiriwa katika lugha arobaini. Watu wa Colgate wanahitajika kusoma, kuelewa, na kufuata Kanuni hizi. Ili kutekeleza ahadi yetu, watu wa Colgate hupokea mafunzo ya Kanuni na hupewa cheti kila mwaka.

Kuafikiana na Kanuni kuna rahisishwa na kutumia uamuzi unaofaa na kutafuta mwongozo wakati maswali yanapoibuka. Kama huna uhakika kuhusu hatua fulani, jiulize yafuatayo:

# MASWALI YA KIMAADILI YA KUTOA UAMUZI

**SWALI:**

Ninaruhusiwa kufanya hivi?

**SWALI:**

Je, ninaweka mfano?

**SWALI:**

Ni sawa kuchukua hatua hii?

**SWALI:**

Je, hatua ni ya halali na inalingana na maadili yetu, Kanuni zetu, Miongozo yetu ya Kanuni za Biashara na sera nyingine?

**SWALI:**

Nitajivunia kuripoti hatua hii kwa mtu ninayemuheshimu?

**SWALI:**

Je, hatua hii itaendeleza sifa ya Colgate kama Kampuni yenye uadilifu?

**SWALI:**

Je, ninaonyesha viwango vya juu vya uadilifu?

**JIBU:**

**Ndiyo,** Endelea.

**Hapana,** Tafadhali shauriana na Shirika Kuu la Kisheria au Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji.

# UHUSIANO WETU NA KILA MMOJA



*Msingi wa uhusiano wetu sisi wenyewe unahitaji uwe wa kuaminiana na kuheshimiana.*

## TUNAJITAHIDI KUWA NA MAHUSIANO YA KIKAZI MAZURI

Katika Colgate, tunajivunia kujitolea kwa nguvu kwa watu wetu na mafanikio bora sana yanoyotokana na kujitolea huko. Lakini kiwango hiki cha mafanikio kinaweza tu kufikiwa katika hali ya kuaminiana, mawasiliano ya uwazi na ukweli, na heshima. Mawasiliano yako yote na wenzako, wasaidizi wako, na wasimamizi wako yanafaa kuchukuliwa kama ushirikiano, ambapo tabia ya kila mtu inaongozwa na kujitolea kupita kiasi ili kudumisha viwango vya maadili ya hali ya juu.

Uhusiano wako na wale unaofanya nao kazi unafaa kuwa kama wa timu inayoshinda. Watu wanaofanya kazi kwa pamoja na kwa kuzingatia seti ya madhumuni ya pamoja ndio nguvu ya msukumo wa biashara yetu. Ili uhusiano wa timu hii ya nguvu kufaulu, kila mtu lazima atimize jukumu lake na awe na uhakika kwamba wenzake watafanya vilevile. Hii kumaanisha kutoa msaada unaohitajika kwa wengine, katika kila kiwango, ili kazi ifanyike. Hakuna mtu yeyote ama kitengo cha biashara ambacho kitaweka malengo yake mbele ya yale ya Kampuni.

Uhusiano wako na wale unaofanya kazi nao unafaa kukuza uadilifu kwa kutoa mfano wa heshima, haki na uaminifu. Kama viongozi, tunawajibika kudumisha viwango vya juu vya utendakazi na kuunda mazingira yanayokuza kazi ya pamoja, heshima na tabia ya uadilifu.

## TUNAKUZA MAWASILIANO YA UWAZI NA UKWELI

Himiza fikira za ubunifu na utungaji na ikiwa wewe ni msimamizi, watendee wasaidizi wadogo kama watu binafsi, ukiwapa uhuru unaohitajika wa kufanya kazi zao. Toa maoni ya kuendelea kuboresha utendaji kazi.

Uhusiano wako na msimamizi wako unafaa uwe wa heshima na uaminifu. Wewe na msimamizi wako ni timu moja iliyo na lengo la kufikia malengo yaliowekewa kwa kitengo chako na Kampuni.

Unajukumu sawa na msimamizi wako kuhakikisha kwamba mawasiliano kati yenu ni ya uwazi na ukweli. Chukua hatua mara nyingi kama iwezekanavyo. Kuwa mbunifu katika kutatua shida. Ushirikiano na ubunifu wako ni muhimu kufikia malengo ya kitengo chako na Kampuni.

## TUNATHAMINI WATU WA COLGATE KAMA RASILIMALI YETU KUBWA ZAIDI

Kujitolea kwa Colgate kuwajali watu kunajitokeza wazi kupitia mipango mbalimbali iliyoundwa kukuza na kutuza mafanikio ya watu binafsi na timu. Unahimizwa kujiendeleza zaidi uwezavyo na utoe usaidizi wa maana kwenye mafanikio ya Kampuni. Mwishowe, ni bidii ya watu wa Colgate walio na vipawa na ujuzi ulimwenguni kote inayowezesha mafanikio ya Kampuni yetu.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea Sera ya Usawa wa Ajira ya Kampuni kwenye ourcolgate.com.

- Tunadumisha mazingira jumuishi ya kikazi na kufikia ubora kwa kuvutia na kudumisha watu kutoka misingi yote ya kijamii katika kikosi chetu cha wafanyakazi.
- Tunapiga marufuku unyanyasaji wa kimapenzi au wa aina yoyote wa watu wa Colgate na mtu yeyote katika mahali pa kazi ama anapofanya biashara ya Kampuni.
- Tunajitahidi kuepuka upendeleo ama mwonekano wa upendeleo katika mahali pa kazi kufuatana na sera na utaratibu uliochukuliwa na Kampuni.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea Sera ya Kuzuia Unyanyasaji ya Kampuni kwenye ourcolgate.com.

Colgate hutoa nafasi ya ajira kwa watu wote wenye sifa husika kwa msingi wa usawa. Kampuni haitabagua dhidi ya mwajiriwa au mwombaji ajira yeyote kwa sababu ya:

Hii inajumuisha, lakini haijazuiliwa kwa, kuajiri, kuandikwa kazi, kupandishwa cheo, kuhamishwa, fidia, mafunzo, kushushwa cheo au kupigwa kalamu.

- Mbari au Jamii
- Rangi
- Dini
- Jinsia au Utambulisho wa Jinsia
- Asili ya Kitaifa
- Umri
- Uelekezo wa Kimapenzi
- Ulemavu
- Hali ya Ndoa
- Hali ya Kuwa Askari Mstaafu
- Sifa bainifu zingine zozote zinazolindwa na sheria

**SWALI:**

Ninaamini kwamba msimamizi wangu huwatedea baadhi ya wanachama wa timu yetu kwa namna isiyolingana na Kanuni zetu za Kusimamia kwa Heshima, lakini sina uhakika. Je, ninaweza kushaurina na mtu kuhusu suala hili kupitia Namba ya EthicsLine?

**JIBU:**

**Ndiyo,** unaweza. Lakini, kumbuka kama una wasiwasi juu ya tatizo lolote la mahali pa kazi, unaweza pia kushauriana na mwakilishi wa Kitengo cha Ajira cha eneo lako au mwanachama anayeaminika wa timu yako ya uongozi. Ikiwa ungependelea, Shirika la Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji liko pia kwa ajili yako ili utafute mwelekeo au ufafanuzi.

**SWALI:**

Mwanachama wa idara yangu amerejelea mara kadhaa uelekezo wa kimapenzi wa mfanyakazi mwenza pamoja na kutumia lugha ya kumshushia heshima. Nilipozungumza nae kuhusu suala hili, alijibu kwamba ilikuwa ni utani tu lakini tabia hiyo imeendelea. Je, nilifanya sawa?

**JIBU:**

**Ndiyo.** Ulifanya sawa kwa Kuongea. Hata hivyo, licha ya juhudi zako nzuri, tabia hiyo ya kukera imeendelea. Ongea na msimamizi wako, Kitengo cha Ajira, Shirika Kuu la Kisheria au Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji kuhusu tabia yoyote ambayo inakiuka Kanuni zetu, sera zetu au kanuni zetu za Kusimamia kwa Heshima.

- Hatuwatumii watoto wadogo kufanya kazi. Kuwafanyisha watoto wadogo kazi hufafanuliwa kama kuajiri mtu yeyoye mwenye umri mdogo kuliko umri uliopitishwa na sheria katika mamlaka ya sheria husika. Hata hivyo, hakuna wakati wowote tutakapoajiri tukijua mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka kumi na sita (16).
- Tunajitahidi kuondoa hatari zinazowa kutokea katika mahali pa kazi na kufuata sheria zote husika za usalama na viwango na sheria za afya.
- Tunasaidia kudumisha zinazoweza salama, mazuri na ya uzalishaji ya kufanya kazi, kwa watu wote wa Colgate na wengine, kwa:
    - kuzuia umiliki, matumizi, uuzaji au uhamishaji wa dawa zisizo halali ama vifaa vya madawa kwa kutumia mali au wakati wa Kampuni;
    - kuzuia kufanya biashara ya Kampuni ukiwa umelewa;
    - kuzuia umiliki au utumizi wa silaha au bunduki, vifaa vya ulipuaji au risasi katika majengo ya Kampuni au unapofanya biashara ya Kampuni kufatana na sheria ya nchi husika. Umiliki wa silaha unaweza kuruhusiwa kwa wafanyakazi wanaolinda usalama wakati umiliki huu umethibitishwa kuwa muhimu ili kuimarisha usalama na ulinzi wa watu wa Colgate;
    - kuzuia matendo yoyote ambayo yanaweza kuchukuliwa kama ya uhasama, kutishia, kushusha hadhi au vitisho; na
    - kuhitaji kwamba tukio lolote la matumizi mabaya ya dawa na vileo katika mahali pa kazi, vurugu au kumiliki silaha kinyume cha sheria kwenye majengo ya Kampuni kuripotiwe mara moja kwa Kitengo cha Ajira, Usalama Mkuu, Shirika Kuu la Kisheria, Maadili na Mwafaka Duniani au usimamizi.

**SWALI:**

Mmoja wa wafanyakazi wenzangu ni mzee kwa hivyo ninajaribu kumsaidia kwa kumrahisishia zaidi kwa kumsaidia na kazi ambazo ninafikiria zinaweza kuwa ngumu kwa mtu wa umri wake. Ninajaribu tu kusaidia lakini hivi karibuni nilisikia kutoka kwa msimamizi wetu kwamba nimemkasirisha Je, tabia hii sio sawa?

**JIBU:**

**Ndiyo.** Hustahili kudhania kwamba kwa sababu ya umri wake mfanyakazi mwenzako hana ujuzi na uwezo sawa nawe. Kumtendea mtu tofauti kwa sababu ya umri wake hakukubaliwi katika mahali pa kazi. Ongea na mweleze kwamba kutaka kwako kumsaidia kulikuwa ni kwa nia ya kumjali na kwamba haukuwa na nia mbaya.

# UHUSIANO WETU NA KAMPUNI




*Kama watu wa Colgate, tunatambua imani na matumaini tuliokabithiwa na tunafanya kazi kwa uadilifu na kwa uaminifu katika hali zote.*

## TUNAEPUKA MIGONGANO YA MASLAHI

Uamuzi ni moja kati ya mali ya thamani zaidi uliyo nayo. Unastahili kuepuka shughuli, maslahi au ushirikiano wowote ambao unagongana na maslahi halali ya Kampuni au unaonekana kuhatarisha kutokuwa na upendeleo au uwezo wako wa uamuzi huru katika kutekeleza biashara ya au na Kampuni. Migongano inaweza kutoka katika hali nyingi. Haiwezekani kuitaja yote hapa, na daima haitakuwa rahisi kutofautisha kati ya shughuli nzuri na isiyo nzuri. Ukiwa na mashaka, wasiliana na Kitengo cha Ajira, Shirika Kuu la Kisheria, Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji au meneja wako kabla ya kuchukua hatua yoyote.

Mwongozo unaofuata hutumika kwa hali nyingi za kawaida za mgongano:

### UWEKEZAJI

Usifanye uwekezaji wowote unaoweza kuathiri uamuzi wako wa kibiashara. Sera za Kampuni zinakataza watu wa Colgate kumiliki hisa ama kuwa na hamu ya kumiliki katika Kampuni inayoshindana na ama inayofanya biashara na Colgate. Kizuizi hiki hakitumiki kwa kumiliki viwango vidogo (kwa ujumla chini ya 1%) vya hisa za Kampuni inayouza hisa kwa umma ila tu uwekezaji huo usiwe wa kiwango kinachoweza kuunda dalili ya mzozo wa upendeleo. Ikiwa ulifanya uwekezaji usiokubaliwa kabla ya kujiunga na Colgate, tafadhali wasiliana na Shirika Kuu la Kisheria.

### FAMILIA

Mjulishe Meneja wako na upate idhini kutoka kwa Mkuu wa Divisheni au Kitengo chako na Shirika Kuu la Kisheria kabla ya kufanya biashara kwa niaba ya Colgate na kampuni yoyote ambayo wewe au mwanafamilia wa karibu ana maslahi.

### KAZI NYINGINE

Usimfanyie kazi mshindani ukiwa bado unafanyia Colgate kazi ama kumfanyia kazi, ama kutoa huduma yoyote kwa, mtu yeyote wa tatu ambaye anaweza kuathiri utendaji kazi ama uamuzi juu ya kazi. Usitumie muda wa Kampuni, vifaa, rasilimali, chapa au nembo kwa kazi ya nje ambayo haina uhusiano na kazi yako hapa Colgate bila kibali kutoka kwa Mkuu wa Divisheni au Kitengo chako.

### MAMBO YA KIBINAFSI

Tunatabua na kuheshimu haki za watu wa Colgate za kushirikiana kwa uhuru na watu wanaohusiana nao katika mazingira ya kikazi, lakini ni lazima tufanye uamuzi mzuri ili kuhakikisha kwamba mahusiano hayo hayaathiri vibaya utendaji wa kazi, uwezo wa kuwasimamia wengine au mazingira ya kazi.

Tabia yoyote ya mahali pa kazi inayotokana na uhusiano wa kimapenzi au urafiki kati ya wafanyakazi inaweza kuwa isiofaa ikiwa tabia hiyo itasababisha mazingira yasiyofaa ya kikazi kwa wengine au dhana ya upendeleo. Upendeleo au kutoa maamuzi ya kibiashara kwa msingi wa mahusiano ya kimapenzi au urafiki badala ya maslahi bora ya Kampuni haviruhusiwi. Watu wanaojikuta katika uhusiano wa kimapenzi au urafiki wanafaa kutoa uamuzi mwema unaowajali wengine.

Msimamizi hastahili kumsimamia mtu ambaye anahusiana naye kimapenzi. Katika hali hiyo, ni lazima wafanyakazi wote wawili waripoti hali hiyo kwenye Kitengo cha Ajira na/au Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji.

Fahamu kwamba mwanafamilia yeyote wa karibu anaweza kuajiriwa katika nafasi ambayo inaweza kusababisha ama kuonekana kusababisha mgonano wa maslahi. Ikiwa hali hii itatokea, muone meneja wako ama mshauri wa sheria wa kitengo chako kwa mwongozo.

### BODI

Pata idhini kutoka kwa CEO na Afisa Mkuu wa Kisheria kabla ya kukubali kutumikia Bodi ya Wakurugenzi ama chama kama hicho katika biashara ya nje ama wakala wa serikali.

Hustahili kutafuta idhini ya kuhudumia Bodi ya shirika lisilokuwa la faida isipokuwa ikiwa shirika hilo lina uhusiano wa kibiashara na Kampuni, ambapo katika hali hiyo unastahili kutafuta idhini kutoka kwa mkuu wa Sehemu au Kitengo chako.

### NADHARI NYINGINE

Tunajitahidi kudumisha mazingira mema ya kazi ambayo yanaangazia maadili ya Kampuni yetu na kukuza mahusiano thabiti ya kufanya kazi. Ijapokuwa migongano ya maslahi mara kwa mara hutokea kutokana na kushughulika na wahusika wa nje, migongano au mwonekano wa mgongano huenda pia ukasababishwa na mahusiano ndani ya Kampuni. Wale kati yetu tunaowasimamia wengine lazima tuwe waangalifu ili kuhakikisha kwamba hali hazijatokea ambazo zinaweza kuonekana kwa wengine kama upendeleo au uwezekano wa mgongano wa maslahi.

Ikiwa una maswali au unajikuta katika hali inayoweza kuwa mgongano wa maslahi, shauriana na meneja wako. Kampuni itashirikiana na wewe ili kushughulikia hali na kutambua suluhu inayofaa.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea maelekezo ya Kampuni yaliyo kwenye Masuala Yanayohusiana na Migongano ya Maslahi ambayo yanaweza kupatikana katika Sura ya 7 ya Maelekezo ya Kanuni za Biashara ya Kampuni yaliyo kwenye ourcolgate.com.

**SWALI:**

Jamaa wa familia yako anamiliki kampuni ya uchimbaji na anawasilisha zabuni ya kufanya biashara katika kituo cha uzalishaji ninapofanya kazi. Ninafanya kazi katika kitengo cha uzalishaji na sina mamlaka yoyote ya kutoa uamuzi. Je, bado nitastahili kuripoti hali hii kama uwezekano wa mgongano wa maslahi?

**JIBU:**

**Ndiyo.** Pamoja na kwamba haudhibiti moja kwa moja matokeo ya mchakato wa zabuni, suala la binamu yako kuwa na mahusiano ndani ya Kampuni linaweza kuonekana kama mgongano wa maslahi. Shauriana na Kitengo cha Ajira, Shirika Kuu la Kisheria au Meneja wako.

## TUNALINDA SIRI ZA BIASHARA NA MAELEZO YA SIRI YA KAMPUNI

Siri za kuuza za Colgate, habari za wamiliki wengine na data ya ndani ni mali ya thamani sana. Siri ya biashara ni maelezo yanayotumika kuhusiana na biashara ya Colgate ambayo kwa ujumla hayajulikani au kutambuliwa kwa urahisi na ni yeti kiushindani. Kwa hivyo, juhudi zimewekwa ili kudumisha usiri wake. Ulinzi wa siri za biashara na maelezo ya siri huchukua jukumu muhimu katika kukua kwetu na uwezo wa kushindana.

### JE, IPI NI BAADHI YA MIFANO YA SIRI ZA BIASHARA AU MAELEZO MENGINE YA SIRI?

- Fomula, muundo, kifaa au maelezo yoyote yanayotumiwa katika biashara yetu ambayo hupatia Colgate faida dhidi ya washindani wake
- Hakimiliki ambayo haijatolewa kwa umma
- Utafiti wa kibiashara
- Mipango mipya ya bidhaa
- Maelezo ya kifedha yasiyo ya umma au maelezo ya upangaji bei ambayo hayajatolewa hadharani
- Michakato ya utengenezaji
- Aina yoyote ya nyenzo zamatangazo au mauzo ambazo hazijatolewa kwa umma
- Maoni ya kisheria au toleo la kazi ya wakili
- Picha au video zisizoidhinishwa zilizopigwa wakati wa utengenezaji wa Colgate au katika kituo cha uchunguzi
- Orodha za wafanyakazi, wateja au wachuuzi
- Maelezo kuhusu mahitaji ya wateja, mapendeleo, tabia na mipango ya biashara

Hata bila kukamilika orodha hii inadokeza sehemu kubwa ya habari inayotakiwa kulindwa. Habari ya siri za kuuza na wamiliki wengine sio lazima ifae kupata hati ya kumiliki, lakini haiwezi kujulikana kwa jumla na umma.

Wajibu wako kuhusu siri za kuuza za Colgate na maelezo mengine ya faragha ni:

**HUSTAHILI** Kufichua habari hii kwa watu wengine wa Colgate kasoro kwa msingi wa "kuhitaji kujua" au "kuhitaji kutumia".

**HUSTAHILI** Kuhusisha wahusika wengine wa nje kushughulikia maelezo haya bila kupitia vidhibiti vya kiusalama vya teknolojia ya habari husika ya wahusika wengine wa nje na bila kuwa na makubaliano yanayofaa ya siri na mhusika mwingine wa nje.

**HUSTAHILI** Kuchapisha au kujadili maelezo haya kwenye tovuti zinazopatikana kwa umma au tovuti za mitandao ya kijamii.

**HUSTAHILI** Kutumia habari hii kwa faida yako au kwa faida isiyoidhinishwa ya watu nje ya Colgate.

**UNASTAHILI** Kuchukua hatua nyingine zote zinazofaa kulinda siri za biashara ya Colgate na maelezo ya faragha.

Iwapo utaondoka Colgate, jukumu lako la kulinda siri za biashara za Colgate na maelezo mengine ya faragha litaendelea. Unapaswa pia kukumbuka kwamba mawasiliano, maudhui yaliyochapishwa, maelezo pepe, hati au rekodi za aina yoyote, utaratibu maalum wa ufahamu, taratibu, njia maalum za Colgate za kutenda - ikiwa ni za siri au la - vyote ni mali ya Kampuni na lazima vibaki Colgate. Lazima urejeshe rasilimali zote za Kampuni ulizonazo, unazosimania au unazodhibiti iwapo utaondoka kwenye Kampuni.

Ikiwa una swali kama habari fulani ni ya umiliki ama ya siri ya kuuza, wasilliana na Shirika la Kisheria la Duniani.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea maelekezo ya Kampuni yaliyo kwenye Kuhifadhi Maelezo ya Umiliki wa Kampuni ambayo yanaweza kupatikana katika Sura ya 12 ya Maelekezo ya Kanuni za Biashara ya Kampuni yaliyo kwenye ourcolgate.com.

**SWALI:**

Kwenye lifti nikielekea eneo langu la kazi, niliwasikia wafanyakazi wenzangu wawili wakijadili kazi wanayoifanya kuhusu bidhaa mpya inayotengenezwa. Nimekuwa na wasiwasi kwa sababu tunashiriki ofisi moja na makampuni mengine na maelezo waliyokuwa wakiyajadili yalionekana kuwa ya siri. Je, ningestahili kusema chochote?

**JIBU:**

**Ndiyo.** Ni muhimu watu wa Colgate wasijadili maelezo ya siri ya Kampuni katika maeneo ya umma kama vile ukumbini, mikahawani, lifti, n.k. ambapo hakufahi kuwa na mazungumzo ya faragha. Unahimiziwa "Kuongea" ili uwafahamishe wafanyakazi wenzako hoja zako na uwajulishe kuhusu hali hii.

## TUNAFUATA SERA ZA WANAHABARI NA VYOMBO VYA HABARI

- Maombi ya kuzungumza kwa niaba ya Colgate kuhusiana na maelezo ya kifedha ya kampuni au biashara kutoka kwa vyombo vya habari, wanahabari, jamii ya kifedha au umma yanapaswa yaelekezwe kwa Makamu wa Rais, Mawasiliano ya Shirika au Makamu wa Rais, Mahusiano ya Wawekezaji.

- Maombi ya kutoa maelezo kwa niaba ya Colgate kwa washirika kutoka kwenye Tume ya Amana na Ubadilishanaji wa Fedha, Soko la Hisa la New York au wasimamizi wengine ulimwenguni kote lazima yaelekezwe kwa Shirika Kuu la Kisheria.

Ni muhimu kwamba mfanyakazi yeyote asijibu kwa niaba ya Kampuni swali lolote kama hilo ama kuwasiliana wenyewe kwa wenyewe kwa sababu majibu yoyote yasiyo sahihi au ya kupotosha, hata kukataa au kukanusha maelezo, kunaweza kusababisha utangazaji usiofaa na kunaweza kuathiri Kampuni vibaya.

Sera hii haitumiki kuuliza hadharani habari ya fedha, kama ya Kila Mwaka na Ripoti za Robo Mwaka, ama shuguli za ukuzaji wa Kampuni hadharani.

Maombi ya mahojiano na mfanyakazi yeyote wa Colgate akiongea kwa niaba ya Kampuni au biashara zake na/au utoaji wa matoleo yoyote ya habari ya kampuni kwa Wanahabari na/au taarifa zozote lazima zipitiwe na kuidhinishwa mapema na Makamu wa Rais, Mawasiliano ya Shirika au Makamu wa Rais au Mahusiano ya Wawekezaji. Mahojiano yanayoanzishwa na Kampuni pia lazima yaidhinishwe kabla ya kupanga kukutana na vyombo vya wanahabari.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea maelekezo ya Kampuni yaliyo kwenye Biashara ya Amana na Siri ya Maelezo, ambayo yanaweza kupatikana katika Sura ya 4 ya Maelekezo ya Kanuni za Biashara ya Kampuni yaliyo kwenye ourcolgate.com.

## TUNATUNZA VITABU NA REKODI SAHIHI ZA KIFEDHA

Hali halisi ya kifedha ya Kampuni yetu na matokeo ya shughuli zake lazima zinakiliwe kulingana na mahitaji ya sheria na kwa ujumla ikubaliwe na kanuni za jumla za kuhesabu (GAAP). Sera ya Kampuni, hata pia sheria, uhitaji Colgate kutunza nakala za kifedha, rekodi na akaunti zinazoangazia kwa usahihi na usawa hali ya mapatano ya biashara na utoaji wa mali ya Kampuni.

Uadilifu wa rekodi za kifedha na uhasibu wa Kampuni hutegemea usahihi na ukamilifu wa maelezo yaliyotolewa ili kuthibitisha maelezo yaliyoingizwa kwenye vitabu vya hesabu vya Kampuni. Kila mtu anayehusika katika kuunda, kuchakata na kurekodi habari kama hizo anawajibika uadilifu wake. Kila rekodi ya uhasibu ya kifedha inapaswa

kuangazia hasa yale yaliyofafanuliwa na nyaraka Hakufai kabisa kuwa na ufichaji wa maelezo kutoka kwa, au na, usimamizi, au kutoka kwa wakaguzi huru au wa ndani ya Kampuni.

Hakuna malipo kwa niaba ya Kampuni ambayo yataidhinishwa au kulipwa ikiwa sehemu yoyote ya malipo hayo itatumiwa kwa lengo lingine lolote kando na ilivyoelezwa katika hati za kuthibitisha malipo. Hakuna rekodi za uongo au za kupotosha zinazostahili kuingizwa katika rekodi zozote za vitabu au za kifedha za Kampuni kwa lengo lolote lile. Hakuna fedha, mali, au akaunti yoyote ya Kampuni inaweza kuanzishwa, kununuliwa au kudumishwa kwa lengo lolote lile isipokuwa kama inaonyeshwa vizuri katika vitabu na rekodi za Kampuni. Hakuna fedha za shirika ama mali zitaruhusiwa kutumiwa kwa sababu yoyote isiyo halali ama isiyo sawa.

Wasimamizi na wengine wanaosimamia uandalizi wa habari za fedha lazima wahakikishe kwamba sera za fedha za shirika la Colgate zimefuatwa. Mapato na matumizi yanapaswa kutambuliwa vizuri na kwa wakati unaofaa.

Mali na dhima inapaswa kurekodiwa vizuri na kuthaminiwa inavyostahilika. Vile vile, wale wanaowajibikia au wanaohusika kujaza rekodi za Colgate na tume ya Amana na Ubadilishanaji wa fedha na rekodi nyingine zinazohitajiwa na sheria husika, au mawasiliano mengine na jamii ya biashara au kifedha, wanapaswa kuhakikisha kwamba taarifa katika rekodi na mawasiliano hayo ni kamili, za haki, sahihi, ya wakati unaofaa na zinaeleweka. Ikiwa utafahamu uwezekano wa kusahaulika, uwongo au rekodi za kifedha kutokuwa sahihi au katika ripoti za Tume ya Amana na Ubadilishaji wa fedha za Colgate au mawasiliano mengine, au tatizo lolote katika udhibiti wa ndani, lazima uripoti mara moja maelezo kama hayo kwa meneja wako au Shirika Kuu la Kisheria. Unaweza pia kuwasiliana na Idara ya Kuu ya Maadili na Utekelezaji ya Kampuni kuhusu masuala haya.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea maelekezo ya Kampuni yaliyo kwenye Hati za Kampuni, ambayo yanaweza kupatikana katika Sura ya 5 ya Maelekezo ya Kanuni za Biashara ya Kampuni yaliyo kwenye ourcolgate.com.

## TUNALINDA MALI YA COLGATE

Mali ya Kampuni, vifaa ama huduma lazima zitumiwe kwa sababu zinazofaa na zilizoidhinishwa. Wizi wa pesa, mali ama huduma haukubaliwi kabisa. Matumizi ya vifaa, mifumo, vituo, kadi za mikopo za shirika la Colgate na ruzuku lazima yahusiane na kazi yako katika Colgate au kwa malengo yaliyoidhinishwa na usimamizi. Unawajibika kibinafsi kulinda mali uliyokabidhiwa na Kampuni, lakini pia kwa kusaidia kulinda mali ya Kampuni kwa ujumla. Unapaswa kuwa mwangalifu kwa hali au matukio yoyote ambayo yanaweza kusababisha hasara, matumizi mabaya au wizi wa mali ya Kampuni na ni lazima uripoti hali zote kama hizo kwa meneja wako au Usalama wa Shirika punde tu unapozifahamu.

**SWALI:**

Je, nifanye nini nikiulizwa kucheleweshа kupata gharama zingine hadi kipindi kingine? Kwa mfano, kama tu atanifafanulia kwamba "maadamu zirekodiwe mwaka huu wa mapato, hatufanyi kitu chochote kibaya," hiyo ni kweli?

**JIBU:**

**Hapana.** Kuchelewesha ulimbikizaji wa gharama kwa maksudi, bila kuzingatia kiasi cha fedha, ni tabia ya kupotosha, isiyokubalika na inayo weza kuwa kinyume cha sheria. Kila shughuli ya kibiashara na kifedha, hata kama ndogo, lazima iripotiwe kwa usahihi na uaminifu. Udanganyifu wowote wa waraka au rekodi ya Kampuni ni kosa baya na linaweza kusababisha ukomeshaji wa ajira.

Ni maafisa fulani wa Kampuni na wafanyikazi wengine wakubwa pekee wanaoruhusiwa kutoa ahadi zinazoathiri mali ya Kampuni. Isipokuwa kama una idhini inayofaa, haustahili kutoa ahadi zozote zinazoathiri mali za Kampuni. Kama una maswali au unahitaji ufafanuzi, unastahili kuwasiliana na mkurugenzi wa kifedha wa eneo au Kitengo chako.

## TUNATUMIA RASILIMALI ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MITANDAO YA KIJAMII KWA UWAJIBIKAJI

Rasilimali za Habari za Teknolojia za Colgate na Mitandao ya Kijamii lazima vitumiwe kwa uwajibikaji na kwa namna zinazolingana na Kanuni na sera na taratibu nyingine zote za Kampuni.

Rasiliamli za kiteknolojia za Colgate hujumuisha vifaa, programu na huduma zote za sasa na za baadaye ambazo hukusanya, kuhifadhi, na kuwasilisha na kuchakata data ambayo inamilikiwa, imeazimwa au kutolewa na Colgate.

Rasiliamli za kiteknolojia za Colgate zinastahili kutumiwa kwa njia ya heshima na ya kitaalamu kwa malengo ya kibiashara ya Colgate tu, isipokuwa kwa matumizi yaliyozuiwa na yanayofaa ya kibinafsi.

Kwa kuongezea, matumizi yafuatayo yamekatazwa:

- Ujumbe wa unyanyasaji, ubaguzi, matusi, utapeli, au wa kutishia, ikijumuisha misingi ya mbari, dini, asili ya kitaifa, jamii, rangi, ngono, utambulisho wa jinsia, umri, uraia, hali ya kuwa askari mstaafu, hali ya ndoa, ulemavu au hali nyingine yoyote inayolindwa na Sheria.

- Usambazaji usiodhinishwa wa maelezo ya siri au ya faragha ya biashara za Colgate au majadiliano yasiyoidhinishwa ya biashara ya kifaragha ya Kampuni au michakato ya kindani ya siri kwenye tovuti yoyote ya nje.

- Kusababisha au kukubali ukiukaji wa usalama au kuvurugwa kwa mtandao wa mawasiliano au/na kufichua kwa njia isiyofaa kitambulisho cha mtumiaji au nenosiri lako kwa wengine ili kuwaruhusu kutumia nenosiri lako.

- Matumizi yoyote mengine yaliyokatazwa na Maelekezo ya Kanuni ya Biashara au Maelekezo kuhusu Kutumia Rasilimali za Teknolojia ya Habari na Mitandao ya Kijamii.

Isipokuwa kama inavyozuiwa na sheria husika, Colgate inahifadhi haki ya kufuatilia na kuhakiki Nyenzo zote za Kiteknolojia ya Kampuni katika hali zinazofaa kulingana na uamuzi wa Kampuni na kulingana na sheria husika. Haki ya kampuni ya kufuatilia, kufikia na kuhakiki Rasilimali zote za Kiteknolojia za Kampuni inahusu maelezo ya kibiashara na hata pia maelezo ya kibinafsi yaliyoundwa, hifadhiwa au pitishwa kwa kutumia Nyenzo za Kiteknolojia za Kampuni, na pia hujumuisha tovuti za mitandao ya kijamii zilizotembelewa kupitia Rasilimali za Kiteknolojia za Kampuni. Wafanyakazi wanapaswa wasitarajie faragha kuhusiana na maelezo ya kibiashara au ya kibinafsi hayo.

Colgate ina haki ya kuzuia au kuondoa upatikanaji kwa mtumiaji yeyote au matumizi ya Nyenzo ya Teknolojia ya Maelezo ya Colgate wakati wowote, kwa sababu yoyote ile, bila ilani ya mapema, isipokuwa inapokatazwa na sheria.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea maelekezo ya Kampuni yaliyo kwenye Kutumia Rasilimali za Teknolojia ya Habari na Mitandao ya Kijamii ambayo yanaweza kupatikana katika Sura ya 13 ya Maelekezo ya Kanuni za Biashara ya Kampuni yaliyo kwenye ourcolgate.com.

# UHUSIANO WETU NA BODI YA WAKURUGENZI



*Tumefanikiwa kuwa na kikundi cha watu wa kipekee wanaotoa huduma kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni, inatoa ushauri, mwongozo, na uongozi ambao ni muhimu sana kwa mafanikio yetu yanayoendelea. Ujuzi wao wa pamoja kwenye biashara, masomo na huduma ya umma, ujuzi wa kimataifa, mafanikio ya kimasomo, maadili ya tabia na anuwai, Bodi yetu ya Wakurugenzi inatoa maono thabiti ya biashara ya Kampuni.*

## TUNA BODI YA WAKURUGENZI AMBAYO IKO HURU, YENYE UJUZI NA INAYOHUSISHA WATU MBALIMBALI

Kujitegemea kunakuza uadilifu na uwajibikaji. Ni sera ya Colgate kuwa na Bodi la Wakurugenzi ambalo kwa asili lina wakurugenzi wanaojisimamia. Wakurugenzi wote wanaohudumia kamati ya Bodi la Wakurugenzi ambalo husimamia ukaguzi, fidia na uongozi na maswala ya kujitegemea. Hakuna ukurugenzi wa kuingiliana, na ni sera ya Kampuni kuwa hakuna yeyote kati ya wakurugenzi wa kujitegemea atakayepokea malipo yoyote ya ushauri, sheria ama malipo yoyote yasiohusika na ukurugenzi kutoka kwa Kampuni.

## TUNAKUZA MAWASILIANO YA MOJA KWA MOJA NA WAZI NA BODI

Nje na ndani ya chumba cha mikutano, wakurugenzi wa Colgate wanawasiliana moja kwa moja na mara kwa mara na usimamizi wa Kampuni. Meneja wakuu mara kwa mara huungana na wakurugenzi wakati wa mikutano ya Bodi na kwa pamoja wanahusika kikamilifu katika mazungumzo mbalimbali ya masuala ya kibiashara. Katikati ya mikutano ya bodi iliyopangwa, wakurugenzi hualika pia, na mara kwa mara huonana na meneja wakiwa na maswali na maoni. Matokea ya mazingira ya uwazi na uaminifu yanaangazia utamaduni wa biashara ya Colgate na yanasaidia bodi kuchukua usukani katika maendeleo na muundo wa muongozo wa biashara ya Kampuni.

## TUNAJITOLEA KUWA NA UONGOZI BORA ZAIDI WA KAMPUNI

Bodi ya Colgate imekuwa kiongozi katika kusaidia kubuni uongozi bora wa Kampuni. Ni moja wapo ya kanuni bunifu ya maadili mema kuongoza shughuli zote za biashara na kukuza mikakati ya Bodi na kamati zake, Colgate imeweka shughuli bora zaidi za uongozi wa Kampuni katika karne mbili zilizopita, ambazo zinaendelea kuboreshwa na kuandaliwa. Bodi la Colgate liko katikati ya sera hizi na linaamini kwamba uongozi mwema wa biashara unaambatana na unasaidia sana mafanikio yetu ya muda mrefu.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea "Maelekezo ya Bodi kuhusu Masuala Muhimu ya Kusimamia Kampiuni," ambayo yanaweza kupatikana kwenye colgatepalmolive.com.



# UHUSIANO WETU NA MASHIRIKA YA BIASHARA MENGINE

*Kila mmoja wetu anawajibika kwa jinsi tunavyooonekana kwa wagavi, wateja na wahusika wengine wa nje. Ni muhimu tudumishe sifa ya Kampuni ya uaminifu na ukweli tunapofanya biashara na makundi haya.*

## TUNAFANYA KAZI NA WAGAVI, WATEJA NA WAHUSIKA WENGINE KWA UADILIFU

Ni muhimu kuwatendea wagavi, wateja na wahusika wengine wa nje kwa uaminifu ili kuwa na uhusiano mwema na wa kudumu kibiashara. Tunawapa wahusika wengine wa nje watarajiwa wote uzingatiaji wa haki na usawa. Maamuzi ya kuwateua wachuuzi hutegemea kigezo cha malengo kama vile bei na ubora, na hata pia uthabiti na uadilifu.

Vile vile, hatuwapendelei kibinafsi wahusika wengine wa nje katika bei, ruzuku ya matangazo, usaidizi kwa matangazo au mambo kama hayo. Uhusiano na wagavi, wateja na wahusika wengine wa nje umejadiliwa zaidi katika sehemu ya Kanuni hii inayohusika na Uhusiano Wetu na Serikali na Sheria.

Kanuni ya Maadili Mema ya Wahusika Wengine ya Colgate inapatikana kwa lugha mbalimbali kwenye tovuti ya Kampuni.

## HATUTOI AU KUPOKEA ZAWADI ZISIZOFAA

Haikubaliwi kutoa, kupeana, au kupokea zawadi, malipo au faida nyingine (pamoja na, lakini bila kukomea kwa hongo au bahashishi) ili kushawishi au kuonekana kushawishi uamuzi wowote wa biashara. Kama unakusudia kutoa, au umetoa, au umepewa au kupokea zawadi, malipo au faida yoyote ambayo ina thamani maalum ya zaidi (ya takriban $50 za Marekani) au kama unaamini zawadi, malipo au faida kama hiyo ilitolewa kwa jaribio la kushawishi uamuzi wa kibiashara, lazima uwasiliane na Shirika Kuu la Kisheria au Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji. Pia, zingatia kwamba huenda ukakubali zawadi tu ya thamani ya kifedha kutoka kwa chanzo kimoja mara moja kwa kila kalenda ya mwaka. Ikiwa itakuwa aibu kwa Kampuni ikiwa hutakubali zawadi inayozidi thamani maalum, basi kukubali kwako kwa zawadi hiyo kunafaa kuripotiwa kwa Shirika Kuu la Kisheria. Isitoshe, usipangie au kupokea zawadi, malipo au faida nyingine ambazo zina thamani maalum kwa niaba ya mjumbe wa karibu wa familia kutoka kwa mtu yeyote ambaye Kampuni ina uhusiano unaoendelea wa kibiashara au ingependa kuanzisha uhusiano wa kibiashara siku za mbeleni.

**Fuata sheria hii:** usitoe au kukubali kamwe zawadi au huduma kama itakushawishi au itaonekana kukushawishi. Hii haijumuishi burudani au zawadi yoyote ya biashara ya mara moja moja ambayo ni ya thamani maalum.

Unafaa kukumbuka kwamba kuna sheria maalumu zinazosimamia tabia inayofaa katika kuhusiana na maafisa wa serikali, jimbo, serikali ya mtaa au serikali ya kigeni ambayo haikubaliani na sheria za kushughulika na vyombo visivyo vya serikali. Kwa ujumla, huwezi kutoa au kuwapa wafanyakazi wa serikali au serikali zawadi, ruzuku au kitu chochote cha thamani, ikiwa ni pamoja na lishe au usafiri, isipokuwa iwe imeidhinishwa mapema na Shirika Kuu la Kisheria.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kuhusu zawadi kwa maafisa wa serikali au serikali, kwa kurejelea Sera za Jumla kuhusu Matumizi Yanayohusiana na Maafisa wa Serikali na Serikali, na Fomu husika ya Idhini.

Wagavi na wachuuzi wa Colgate wanapaswa wakati wote kushauriwa kuhusu mahitaji ya kufuata Kanuni ya Maadili Mema ya Wahusika Wengine wakati wanafanyakazi na sisi au wakabiliane na uwezekano wa kupoteza biashara yetu kwa kushindwa kufanya hivyo. Vile vile, tunapaswa kuheshimu na kufuata sera za wateja au wagavi ili mradi hazipingani na za kwetu wenyewe.

**SWALI:**

Mteja alinialika kwa mashindano ya kulipwa ya gofu. Nilimwarifu msimamizi wangu kuhusu mwaliko huo na akakubali kuhusika kwangu ili mradi masuala ya biashara yajadiliwe. Wakati wa mashindano hayo, bahati nasibu ilichezeshwa na nilishinda seti ya vifaa vya gofu ambavyo vinazidi thamani maalum. Je, nitakuwa nikikikuka Kanuni nikivikubali?

**JIBU:**

**Ndiyo.** Zawadi yoyote iliyopokelewa katika mashindano au kuchezeshwa bahati nasibu itachukuliwa kuwa zawadi. Kama thamani ya zawadi inazidi thamani maalum iliyoelezwa katika sera yetu ya zawadi, kuikubali kutachukuliwa kama ukiukaji wa Kanuni. Pia, Namba ya EthicsLine inaweza kutoa maelekezo au ushauri zaidi ikiwa una maswali.

## TUNAHESHIMU SIRI ZA BIASHARA NA MAELEZO YA SIRI YA WENGINE

Ni sera ya Colgate kutokiuka kimaksudi haki za ufahamu wa kiakili wa mali ya wengine. Pia ni sera ya Kampuni kuheshimu siri za uuzaji au habari za wamiliki za watu wengine. Hii ni muhimu hasa ikiwa utajiunga na Colgate na una ufahamu wa siri za biashara au maelezo ya umiliki kutoka kwa mwajiri wako wa awali. Ikiwa maswali yoyote yatatokea katika eneo hili, shauriana na Shirika la Kisheria Duniani.

Ikiwa mtu yeyote nje ya Kampuni atakujia na uvumbuzi, ugunduzi au wazo, ni muhimu ulinde Kampuni dhidi ya ukiukaji wa baadaye au madai ya kifedha. Usiruhusu watu wa nje kufichua maelezo yoyote ya uvumbuzi, ugunduzi au wazo lao jipya kwako bila kwanza kushauriana na Shirika Kuu la Kisheria. Waelekeze watu wote wanakujia na mawazo yasiyoombwa ama kwa Shirika Kuu la Kisheria au Idara ya Masuala ya Wateja katika eneo lako ili wayashughulikie kulingana na utaratibu wa Kampuni.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea maelekezo ya Kampuni yaliyo kwenye "Kuhifadhi Maelezo ya Umiliki wa Kampuni na Kuheshimu Maelezo ya Umiliki ya Wengine" ambayo yanaweza kupatikana katika Sura ya 12 ya Maelekezo ya Kanuni za Biashara ya Kampuni yaliyo kwenye ourcolgate.com.

# UHUSIANO WETU NA WATUMIAJI



*Sifa ya Kampuni yetu imejengwa juu ya ubora na usalama wa bidhaa zetu. Kujitolea kwetu kwa ubora na usalama ni muhimu katika kuendeleza ukuaji na mafanikio ya Kampuni.*

## TUNAWEKA VIWANGO VYA JUU ZAIDI KWA BIDHAA ZETU

Tumejitolea kuhakikisha kwamba watumiaji wanaweza kuamini bidhaa za Colgate kwa utegemeaji, ubora na utendaji wa kiwango cha juu. Pamoja na kutumikia mabilioni ya watu katika masoko ambayo tunafanya kazi, ni lazima tujitahidi kuzalisha bidhaa zetu kwa njia nzuri zaidi ili ziweze kuwa za bei nafuu kwa idadi kubwa zaidi ya wateja.

Bidhaa zinazouzwa na Colgate sio lazima tu zitimize viwango vya usalama vilivyowekwa na sheria, lakini pia mara kwa mara viwango vikali zaidi vya Kampuni. Tunahusika katika mipango ya kutoa msaada wa haraka kwa watumiaji katika shutuma za bidhaa zilizoharibiwa au kutumiwa vibaya au ghushi. Afya, usalama na maslahi ya mtumiaji vina muhimu wa msingi kwetu na ukiwa kama mfanyakazi wa Colgate ni jukumu lako kupiga ripoti kuhusu masuala yoyote unayokumbana nayo yanayohusiana na ubora au usalama wa bidhaa kwa kiongozi wa kitengo cha biashara.

Kwa maelezo ya ziada kuhusu usalama wa viambato vyetu, tafadhali rejelea sera yetu kuhusu Usalama wa Viambato ambayo inaweza kupatikana kwenye colgatepalmolive.com.

## TUNAWAJIBU WATEJA WETU

Kwa sababu biashara yetu ni bidhaa za utumiaji, mafanikio yetu yanategemea kuridhika kwa mtumiaji, uaminifu na maslahi mema. Tunaweza kufikia vizuri malengo yetu na kutumikia mahitaji ya watumiaji kwa kufuata kipindi thabiti, cha haki na nyeti na cha kujali mawasilainao ya watumiaji.

Tunatambua umuhimu wa kutabiri na kujibu mahitaji na mapendeleo ya wateja. Tunaamini kwamba maoni ya watumiaji, hoja na maswala yanayowasilishwa kwenye Kampuni kuhusu bidhaa zetu ni njia muhimu ya kupata habari. Mahitaji ya wateja hubadilika kila wakati, kwa hivyo lazima tuendelee kusikiliza yale watu wanayotaka ili kukidhi mahitaji yanayobadilika.

Wakati mteja anapoonyesha kutoridhika, timu yetu ya Masuala ya Wateja itashughulikia tatizo hilo mara moja, kwa heshima na haki, na kufanya juhudi zote zinazofaa kudumisha au kurejesha sifa yetu njema aliyonayo mteja.

## UTANGAZAJI WETU NI WA KWELI NA SAHIHI

Hali moja iliyo muhimu sana katika biashara yetu ni kutangaza. Utangazaji unafaa kuwa wa ubunifu na ushindani, lakini pia uwe wa kweli, sahihi, na daima ufuate sheria husika. Utangazaji wetu lazima pia uepuke kuwafafanua watu kwa mitazamo potofu kwa misingi kama vile:

- Mbari
- Dini
- Asili ya Kitaifa
- Jamii
- Jinsia au Utambulisho wa Jinsia
- Umri
- Uelekezo wa Kimapenzi
- Hali ya Kuwa Askari Mstaafu
- Hali ya Ndoa
- Ulemavu
- Sifa bainifu zingine zozote zinazolindwa na sheria

**SWALI:**

Mfanyakazi mwenza ni Opereta wa Mashine ambaye anawajibika kutekeleza ukaguzi wa kila saa wa uzani ili kuhakikisha kiwango sahihi cha bidhaa kimetolewa. Ninaamini kwamba hafanyi ukaguzi huu na anaghushi nyaraka zake. Je, ninastahili kumwarifu msimamizi wangu?

**JIBU:**

**Ndiyo.** Sifa ya Kampuni yetu imejengwa juu ya ubora na usalama wa bidhaa zetu. Ikiwa unahisi kwamba hatua zozote zilizochukuliwa zinaweza kuchafua sifa za Kampuni yetu au kuathiri wateja au watumiaji wetu, unastahili kuarifu usimamizi wetu na namba ya EthicsLine mara moja.

Utangazaji unabuni zaidi ya taswira ya bidhaa. Unajenga sifa yetu ya utegemeaji, kutegemewa na uaminifu.

Pia, tuko makini katika kuteua vyombo vya habari ambavyo vitaonyesha ujumbe wetu. Haturuhusu matangazo yetu kuonekana kwenye vipindi vya televisheni au kwenye vyombo vya habari ambavyo vinaruhusu hongo au kutumia sana vurugu au ngono, au tabia nyingine zisizokubalika katika jamii au zinaathiri sifa za bidhaa za Kampuni yetu.

Tunazingatia viwango vya haki vya kibiashara katika kuunda, kutumia na kuchagua utangazaji, alama za biashara, na miundo ili bidhaa zetu zifanikiwe kwa nguvu ya ubora na sifa zake, badala ya kuiga au kufanya biashara kwa ukarimu wa washindani wetu. Haki ya biashara inahitaji:

- Kufuata kwa umakini mahitaji ya sheria ya nchi husika kuhusiana na ukiukaji wa alama za biashara na mashindano yasiyo ya haki.
- Kuepuka kuiga alama za biashara zinazojulikana, misemo, mada na michoro ya utangazaji inaotumiwa na Kampuni za kimataifa na washindani wa ndani.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea maelekezo ya Kampuni yaliyo kwenye Utangazaji, ambayo yanaweza kupatikana katika Sura ya 14 ya Maelekezo ya Kanuni za Biashara ya Kampuni yaliyo kwenye ourcolgate.com.

# UHUSIANO WETU NA SERIKALI NA SHERIA

*Tunatii sheria zote ambazo zinahusu Colgate. Ni sera yetu kuzidisha matakwa ya kisheria na kuafikiana na malengo yake. Daima wasiliana na Shirika Kuu la Kisheria iwapo ukiwa na shaka.*

## TUNATEKELEZA SHERIA ZOTE HUSIKA

Watu wa Colgate lazima waendeshe shughuli za Kampuni kwa kufuata sheria za nchi ambako wanafanya kazi, pamoja na sheria husika za Marekani kama ilivyoelezwa katika Maelekezo, sera na taratibu za Kanuni za Biashara za Kampuni. Kwa kawaida, sisi kama Kampuni tunazingatia viwango vya juu zaidi vinavyostahili. Ikiwa unaamini kuna mgongano kati ya sheria za nchini na sheria husika za Marekani au sera ya Kampuni, tafadhali shauriana na Shirika Kuu la Kisheria.

## TUNATEKELEZA SHERIA ZA USHINDANI

Colgate na wafanyakazi wake duniani kote lazima wafuate kikamilifu sheria za ushindani (zinazojulikana kama sheria za ukiritimba nchini Marekani) ambazo zinatumika katika kila nchi, jimbo na eneo ambako tunafanya kazi. Lengo la sheria hizi ni kuwalinda wateja au makampuni mengine kwa kuhakikisha kwamba makampuni yanashindana kwa haki kwa kutoa bei za chini, bidhaa bunifu zaidi na huduma bora zaidi na kwamba makampuni hayaingiliani na kanuni za soko za ugavi na hitaji. Karibu kila nchi inatumia sheria za ushindani. Ni jukumu letu kufahamu sheria za ushindani ambazo zinatumika mahali tunapofanya kazi na kutafuta mwongozo ukihitajika kutoka kwa Shirika Kuu la Kisheria.

Sheria za ushindani duniani kote zinazuia makubaliano yoyote kati ya washindani ambayo yanaweza kuathiri ushindani. Ufunguo wa makubaliano ni kujitegemea. Colgate lazima iwe huru katika shughuli zake mbalimbali za biashara:

- Upangaji wa bei
- Mapunguzo au matangazo
- Masharti ya ununuzi na mauzo
- Kuchagua wateja, wasambazaji au wagavi
- Chaguo za bidhaa za kuzalisha na bei za kuuzia

Ni muhimu kukumbuka kuwa makubaliano yasiyo ya kisheria hayana hati rasmi na hayahitaji hata kuandikwa. Yanaweza kuwa makubaliano ya mdomo au yanaweza kuwa yanaeleweka kwa namna biashara inavyoendeshwa au kutokana na maoni yanayotolewa kienyeji. Pia, sio lazima mkataba uhitimishwe kuwa kinyume na sheria.

Huenda uhuru wa makampuni ukaathiriwa, na huenda makubaliano yaliyo kinyume na sheria yakahitimishiwa kwa kueleweka, wakati washindani wanapopeana au kupokea maelezo ya siri au yasiyo ya umma kuhusu mipango ya sasa au ya baadaye ya biashara (k.m. ongezeko lililopangwa la bei, gharama za wagavi, uzinduzi wa bidhaa mpya, n.k.). Hii ni muhimu kuzingatia hasa wakati wa uchunguzi wa vyama na mikutano ya biashara. Kwa ujumla, lazima upate idhini kutoka kwa Shirika Kuu la Kisheria kabla ya kushiriki katika mkutano wowote ambako mshindani anaweza kuwepo. Hustahili kamwe kutoa maelezo ya siri ya Kampuni na washindani. Ukipokea maelezo kuhusu mshindani ambayo unaamini yanaweza kuwa ya siri, ni lazima uarifu Shirika Kuu la Kisheria mara moja. Hustahili kutumia au kutoa maelezo haya bila kupokea idhini ya kisheria kwanza.

Sheria za mashindano hulinda pia dhidi ya matendo ya uporaji au yasiyo ya haki ya kampuni zenye nguvu ili kuhakikisha kwamba nafasi ya mashindano ni wazi na ya haki kwa wote. Matendo ambayo yanaweza kuwa halali kama yakiwa ya kampuni zisizo za nguvu yanaweza kuchukuliwa kama kinyume cha sheria kama yakichukuliwa na washindani wenye nguvu. Katika nchi ambazo Colgate ina mgao mkubwa sana wa soko, lazima uwasiliane na mwakilishi wa kisheria wa eneo lako ili kukikisha kwamba hatua fulani zinazokusudiwa (k.m., sera fulani ya kupunguza bei au kukataa kuuza) hazitachukuliwa kama kutumia vibaya nafasi ya nguvu.

Sheria za mashindano pia zinaweka vizuizi fulani katika uhusiano kati ya wagavi na wateja na wasambazaji wao. Katika nchi nyingi, jaribio lolote la kuwanyima wateja au wasambazaji uhuru wao wa kuamua bei au sheria na masharti ya uuzaji, au kuzuia haki zao kufanya kazi kwa uhuru linakiuka sheria za mashindano. Ni muhimu kusisitiza kwa wateja wetu kwamba "Bei yetu Inayopendekezwa ya Mauzo ya Rejareja (au ya Kuuza)" huwa hivyo tu - inayopendekezwa. Wateja wako huru wakati wote kuuza kwa bei yoyote wanayoichagua.

Matokeo ya kukiuka sheria za ushindani huwa makali sana na yanaweza kusababisha faini kubwa kwa Kampuni na adhabu (pamoja na kifungo) kwa watu wowote wanaohusika. Hata uchunguzi wa uwezekano wa kuwepo mwenendo wa kuzuia ushindani unaweza kusababisha uharibifu mkubwa wa sifa na kuvuruga biashara.

Ikiwa una shaka lolote kuhusu hatua unayotarajia kama inaweza kuzua matatizo chini ya sheria ya ushindani, unastahili kuwasiliana na Shirika Kuu la Kisheria.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea maelekezo ya Kampuni yaliyo kwenye Ushindani wa Kimataifa, ambayo yanaweza kupatikana katika Sura ya 6 ya Maelekezo ya Kanuni za Biashara ya Kampuni yaliyo kwenye ourcolgate.com.

**SWALI:**

Mwenzi wa biashara alinieleza kuhusu mkutano ambao unafanywa na mmoja wa washindani wetu wa moja kwa moja wakati wa mkutano wa mambo ya meno. Ningependa kuhudhuria mkutano wao, lakini ninaogopa hawataniruhusu wakijua nimetoka kampuni shindani. Ninaweza kuhudhuria iwapo niweke kitambulisho changu siri?

**JIBU:**

**Hapana.** Sio vizuri kujificha ili usijulikane ili upate maelezo kutoka kwa mshindani. Unapaswa kuwasiliana na Shirika la Kisheria Duniani kabla ya kuhudhuria mkutano wowote wa mshindani, kwa sababu mikutano kama hiyo inaweza kuibua masuala ya kutokukiritimba.

## TUNATEKELEZA SHERIA ZA USALAMA

Wakati mwingine unaweza kuwa na maelezo kuhusu Colgate au makampuni mengine katika soko la hisa ambayo Colgate hufanya kazi nayo ambayo hayajulikana kwa umma ("maelezo yasiyo ya umma") - kama vile matokeo ya kifedha au ya shughuli, uwezekano wa kuungana au kununuliwa, au uwekezaji au ufadhili, mipango ya matangazo au kuletwa kwa bidhaa mpya.

Maelezo huchukuliwa kuwa siyo ya umma hadi yatakapo tangazwa wazi kwa umma - kwa maneno menigne, hadi maelezo yametangazwa kwa upana na muda wa kutosha umepita kuruhusu soko la amana kujibu kuhusu habari hiyo. Ikiwa maelezo haya yasiyo ya umma yanaweza kuzingatiwa kuwa ya "kweli" - yaani, maelezo ambayo mwekezaji mwenye busara atatilia maanani wakati wa kufanya uamuzi wa uwekezaji – basi lazima ufuate sheria zifuatazo za amana na sera ya Kampuni:

- Hustahili kamwe kufanya biashara kwa akaunti yako mwenyewe au kwa akaunti ya mtu mwingine biashara ya hisa, au dhamana au amana nyingine za Kampuni (Colgate au nyingine) ambayo maelezo yasiyo ya umma yanahusiana nayo;
- Hustahili kuhimiza au kuwalazimisha wengine, kwa msingi wa maelezo hayo yasiyo ya umma, kuhusika katika hisa, dhamana au amana nyingine nyingine kama hizo za kampuni;
- Hustahili kufichua maelezo kama hayo yasiyo ya umma kwa watu nje ya Colgate; na
- Usijadili maelezo kama hayo yasiyo ya umma na watu wa ndani wa Colgate isipokuwa kama wana hitaji la kujua maelezo kama hayo.

Kwa maneno mengine, huwezi kutumia maelezo yoyote yasiyo ya umma ambayo unapata kupitia ajira yako na Colgate ili kufaidika mwenyewe au kufaidisha wengine kwa shughuli yoyote ya amana au uwekezaji.

Ukipata habari zozote zisizo za umma kupitia kazi yako Colgate, ni lazima uwe makini kulinda siri ya habari hizo, na hustahili kamwe kuendesha biashara yoyote (au kumshauri mtu mwingine yeyote kuendesha biashara zozote) za amana za Colgate au makampuni yoyote yanayoathiriwa hadi muda unaofaa upite baada ya maelezo hayo kutangazwa hadharani. Kizuizi hiki kinajumuisha shughuli za chaguo za hisa na maamuzi yoyote ya kuwekeza katika au kuuza hisa za Colgate kupitia mipango ya faida ya Kampuni.

Jukumu lako la kudumisha siri ya maelezo yasiyo ya umma litaendelea baada ya ajira yako na Colgate kuisha hadi maelezo hayo yatakapo tangazwa ipasavyo kwa umma.

Ukiwa una swali kuhusu kama maelezo ni "muhimu" au yamefichuliwa kabisa kwa umma, lazima uwasiliane na Shirika Kuu la Kisheria na lazima ujiepushe na biashara ya amana hizo zilizoathiriwa au kutangaza habari hadi utakapo pewa idhini ya kisheria.

**SWALI:**

Ninajua kwamba siwezi kununua au kuuza hisa za Kampuni kulingana na maelezo ya kindani, lakini ninaweza kumshauri mmoja wa familia au rafiki kufanya hivyo?

**JIBU:**

**Hapana.** Utakuwa ukikiuka sheria za biashara ya kidani kama vile ungekuwa ukinunua hisa wewe mwenyewe. Kwa kuongezea, mtu uliyemshauri anaweza kuwa anakiuka sheria kama atajua mapendekezo yako yalikuwa ya maelezo ya kindani.

## TUNATEKELEZA SHERIA DHIDI YA KUTOA HONGO

Kujitolea kwa Colgate kushughulika kisheria na kwa uadilifu na serikali inatumika uliwenguni kote. Sera ya Kampuni na pia Sheria ya Kanuni za Ufisadi wa Kigeni Marekani ("FCPA") na sheria nyingine kama hizo za kuzuia hongo duniani kote huwakataza watu au mtu yeyote anayetenda kwa niaba yetu kuhusiana na biashara yetu kutoa kitu chochote chenye thamani moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa afisa yeyote wa serikali ili kupata biashara yoyote au kuathiri sheria au uamuzi wowote wa kiserikali.

Sera ya kampuni na sheria nyingine husika hukataza pia uwezeshaji au malipo yoyote ya "kurahisisha" kulipwa kwa maafisa wa serikali, iwe moja kwa moja au kwa namna isiyo ya moja kwa moja, ili kuharakisha huduma au kazi yoyote rasmi (kwa mfano, malipo madogo yanayotolewa kwa afisa ili kuhakikisha maombi ya Colgate yako mbele ya mstari au kufupisha muda ambao huduma au hatua nyingine hutolewa). Ada yoyote rasmi iliyo na ithibati ya risiti zilizotolewa na serikali haichukuliwi kama malipo yasiyofaa.

Ili kuhakikisha kwamba hukiuki kiwango hiki, kwa njia ya moja kwa moja au kupitia mhusika mwingine, ni sera ya Kampuni kwamba, kasoro ada zilizowekwa kisheria zilizo na idhibati ya risiti rasmi (k.m., ada za kibali au leseni), hakuna malipo, burudani, usafiri, zawadi au vitu vingine vya thamani vinavyoweza kutolewa kwa maafisa wa serikali, bila kujali kiwango cha thamani, isipokuwa kama imeidhinishwa kabla kwa maadishi na Shirika Kuu la Kisheria.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo kwa kurejelea Sera za Jumla kuhusu Matumizi Yanayohusiana na Maafisa wa Serikali na Serikali, na Fomu husika ya Idhini.

Ni muhimu kujua kwamba neno "maafisa wa serikali" hufasiliwa kwa ujumla na huwajumuisha watu ambao wameajiriwa na taasisi au shirika lolote la umma au linalohusiana na serikali au mtu anayefanya kazi rasmi kwa njia yoyote ile, iwe kwa muda wote, muda maalum au bila kulipwa. Maafisa wa serikali wanaweza kupatikana katika kila tawi na kiwango cha serikali na maisha ya umma na wanaweza kujumuisha wafanya kazi wa forodha wa ngazi za chini hadi watungaji sheria wa ngazi za juu, na hata pia maprofesa na waalimu, daktari wa meno, daktari wa wanyama, au wataalamu wengine na Viongozi wengine Wakuu na wafanyakazi wa vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali. Ikiwa una shaka kama mtu anaweza kufasiliwa kama afisa wa serikali, unastahili kuwasiliana na Shirika Kuu la Kisheria.

Kuwa wa moja kwa moja na mwenye ukweli unaposhughulika na kuwasiliana na wafanyakazi wa serikali. Taarifa yoyote ya uongo ya makusudi inayotolewa kwa wafanyakazi wa serikali (ya mdomo au maandishi) inaweza kukusababishia wewe na Kampuniadhabu kali.

Sheria nyingine za kushawishi zinaweza kuhitaji Kampuni na/au wafanyakazi wake au wahusika wengine kujiandikisha na kuripoti kama mshawishi ikiwa mtu wa Colgate au wakala atawasiliana na mfanyakazi wa serikali kwa lengo la kushawishi sheria kupitishwa au hatua nyingine rasmi. Ikiwa unahusika katika shughuli yoyote kama hiyo au una mipango ya kufanya hivyo, kwa njia ya moja kwa moja au kupitia mhusika mwingine, ni lazima uwasiliane na Shirika Kuu la Kisheria ili ubainishe mahitaji husika pamoja na hatua zinazofuata.

**SWALI:**

Ninafahamu kwamba kuna sheria ambazo zinazuia hongo kwa maafisa wa serikali. Lakini sheria hiyo pia inazuia hongo kwa watu ambao sio maafisa wa serikali?

**JIBU:**

**Ndiyo.** Kuna sheria dhidi ya hongo ambazo zinazuia hongo kati ya wahusika binafsi wa kibiashara; k.m., hongo ya kibiashara. Sheria hizi ni muhimu pia - na zinatekelezwa kabisa - kama zile zinazozuia hongo kwa maafisa wa serikali. Daima kumbuka kwamba sera ya Kampuni na sheria za nchini zinakataza kumhonga yeyote anayefanya kazi ya Kampuni, awe afisa wa serikali au mtu binafsi.

Kando na kukataza hongo kwa maafisa wa serikali, sera ya Kampuni na sheria husika pia hukataza hongo kwa wahusika wa kibinafsi. Hupaswi kutafuta kushawishi uamuzi au tabia ya mhusika yeyote wa nje ambaye unaweza kuwa unafanya biashara ya Kampuni naye kwa kuahidi zawadi, malipo au faida nyingine, au kwa ushawishi wowote usio wa kisheria.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea maelekezo ya Kampuni yaliyo kwenye Mahusiano ya Kibiashara na Vyombo vya Serikali, ambayo yanaweza kupatikana katika Sura ya 10 ya Maelekezo ya Kanuni za Biashara ya Kampuni yaliyo kwenye ourcolgate.com.

## TUNATEKELEZA SHERIA ZA BIASHARA ZA KIMATAIFA

Kampuni huzingatia sheria zote husika zinazosimamia biashara ya kimataifa na lazima pia izingatie masharti ya biashara ya Marekani bila kujali eneo tunapofanyia kazi duniani.

Sheria za Vikwazo vya Biashara husimamia uagizaji na mauzo ya nje na huenda pia zikazuia Kampuni kufanya biashara na baadhi ya nchi au watu au vyombo fulani. Kabla ya kufanya kazi na mtu mwingine wa nje yeyote (mchuuzi, mteja, n.k.), mtu huyo mwingine wa nje lazima akaguliwe katika orodha mbili za "Watu Waliozuiliwa" zinazohifadhiwa na serikali ya Marekani ili kuhakikisha kwamba Kampuni iko huru kuendelea na shughuli.

Kampuni hairuhusiwi kuhusika na ususiaji wa kigeni ambao haujaidhinishwa na Marekani na inapaswa kuripoti mara moja maombi yoyote yanayohusiana na ususiaji. Maombi yoyote kama hayo lazima yaripotiwe mara moja kwa Shirika Kuu la Kisheria ili kushughulikiwa ipaswavyo.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea maelekezo ya Kampuni yaliyo kwenye Shughuli za Biashara za Kimataifa, ambayo yanaweza kupatikana katika Sura ya 9 ya Maelekezo ya Kanuni za Biashara ya Kampuni yaliyo kwenye ourcolgate.com.

## TUNATEKELEZA SHERIA ZA FARAGHA YA DATA NA ULINZI WA DATA

Colgate uheshimu faragha ya wafanyakazi, watumiaji, wateja, wagavi na watu wengine wa nje ambao wana uhusiano wa kibiashara na Colgate na kwa hivyo, tunashughulikia data ya kibinafsi kwa kuwajibika na kulingana na sheria zote husika za faragha ya data na ulinzi wa data.

Kama sehemu ya ajira yao na Colgate, huenda wafanyakazi wakatoa maelezo mengine ya kibinafsi kwa Kampuni, kama vile anwani za nyumbani na barua pepe, maelezo ya familia kwa malengo ya faida, na maelezo mengine ya kibinafsi.

Vivyo hivyo, watumiaji wetu, kupitia maombi ya maelezo ya bidhaa au kuhusika katika mashindano yaliyodhaminiwa ya Kampuni, huenda wakatoa maelezo ya kibinafsi, kama vile majina, anwani za mtaa na anwani za barua pepe kwa Kampuni.

Wakati wa mahusiano ya kibiashara na Colgate, wateja, watoa huduma na watu wengine wanaweza kutoa maelezo ya kibinafsi, kama vile majina, nambari za simu, nambari za faksi, anwani za mtaa, anwani za barua pepe na maelezo ya kadi ya mkopo, kwa Kampuni.

Kwa kuzingatia maelezo haya yote, ni sera ya Colgate:

- Kukusanya, kuchakata, kutumia na kuweka data za kibinafsi kwa sababu pekee zilizotolewa kwetu, kasoro kama tumepata kibali cha matumizi mengine, na kama inavyofaa kwa malengo yetu ya kuweka rekodi;
- Kuchukua hatua zote zinazofaa ili kulinda data za kibinafsi ili kuzuia ufichuzi au matumizi yasiyoidhinishwa;
- Kutotoa data za kibinafsi kwa watu wengine wa nje kasoro watoa huduma wetu wengine ambao hutusaidia katika kusimamia bishara yetu na hapo tu kama mhusika huyo amekubali kuafikiana na viwango vyetu vya faragha na hata sheria zote husika za faragha;
- Kuzingatia sheria zote husika za faragha.

Sheria zinazohusiana na faragha za data na ulinzi wa data zinakuzwa na kurekebishwa mara kwa mara. Tumejitolea kufuatilia sheria zinazobadilika za faragha ya data na ulinzi wa data na tunaweza, mara kwa mara, kukuza sera maalum zinazohusiana nazo.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea maelekezo ya Kampuni yaliyo kwenye faragha za data na ulinzi wa data ambayo yanaweza kupatikana katika Sura ya 11 ya Maelekezo ya Kanuni za Biashara ya Kampuni yaliyo kwenye ourcolgate.com.

## TUNATEKELEZA SHERIA ZA KUWEKA REKODI

Sheria nyingi duniani zinahitaji kwamba Colgate iweke aina fulani za rekodi (pamoja na hati halisi na data pepe) kwa muda maalum. Kushindwa kuzingatia mahitaji haya kunaweza kufanya Kampuni ipigwe faini kubwa na adhabu nyingine. Colgate imejitolea kwa Mpango wa Kudhibiti Rekodi ambao unaafiki sheria zote husika na mahitaji ya kisheria, huridhisha mahitaji ya kulinda maelezo ya biashara yetu, na huhakikisha kwamba rekodi zilizopitwa na wakati au zisizofaa pamoja na hati nyingine zimetupwa kwa njia inayofaa.

Unahitajika kufichua maelezo au hati muhimu na zinazofaa katika hatua yoyote ya kisheria, uchunguzi au kesi kama inavyohitajika kisheria. Baada ya kupokea hati yoyote ya kuitwa mahakamani, agizo la mahakama au mchakato wowote wa kisheria unaohitaji ufichuzi wa maelezo ya au nyakaka za Kampuni, unahitajika kuarifu Shirika Kuu la Kisheria, kwa kiwango kinachoruhusiwa na sheria.

Katika hali kama hizo, ni lazima ufuate maagizo yote yanayotolewa na Shirika Kuu la Kisheria na utunze rekodi zote ambazo zinafa kwa mashtaka au uchunguzi, bila kujali mahitaji ya Mpango wa Kutunza Rekodi. Usiharibu au kubadilisha rekodi kama hizo, kwani kuharibu rekodi kunaweza kuwa na athari kubwa – pamoja na adhabu kutokana na kesi za madai na /au jinai na  athaari za kiajira kwako pamoja na Kampuni.

**SWALI:**

Ninawezaje kubainisha muda ambao lazima niweke rekodi za Kampuni na ni wakati ninapoweza kuzitupa?

**JIBU:**

Tafadhali angalia tovuti ya Kudhibiti Rekodi za Kampuni katika OurColgate.com > Tovuti za C-P > Shirika Kuu la Kisheria na Udhibiti > Mpango wa Kudhibiti Rekodi au wasiliana na Msimamizi wa Rekodi wa eneo lako (ikiwa inatumika).

Ikiwa una swali kama rekodi Fulani inahusiana na udadisi au mashitaka, wasiliana na Shirika la Kisheria Duniani kabla ya kutupa rekodi hiyo. Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea "Sera ya Mpango wa Kudhibiti Rekodi."

## HATUTOI MICHANGO YA KISIASA

Hakuna fedha au mali ya Kampuni inayoweza kutumiwa kama michango kwa chama chochote cha kisiasa katika nchi yoyote, kwa kiwango chochote cha serikali. Mchango wa kisiasa unajumuisha wa moja kwa moja (pesa) na michango isiyo ya kifedha. Michango isiyo ya kifedha hujumuisha ununuzi wa tiketi za uchangishaji, mchango wa bidhaa, kazi ya kujitolea kwa watu wa Colgate wakati wa saa za kawaida za biashara na utumizi wa vifaa vya Colgate kwa kusaidia mchango au sababu za kisiasa. Ikiwa una swali kuhusu mchango unaokusudiwa wa kisiasa, tafadhali wasiliana na Shirika Kuu la Kisheria.

Kampuni hairuhusiwi kumfidia au kumrejeshea pesa mtu yeyote wa Colgate ama mtu anayehusika na Kampuni (pamoja na washawishi wa nje au watu wengine wa nje), wanaohusika moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja, kwa hali yoyote, kwa michango ya kisiasa.

Watu binafsi wa Colgate watabaki huru kutoa msaada wa kibinafsi kwa wagombeaji ama vyama watakavyo chagua. Mchango wa kibinafsi ni jukumu na mzigo wa mtu binafsi na haupaswi kufanywa kwa lengo la kusaidia Colgate au makampuni yake tanzu kwa njia yoyote ile.

Kama makampuni mengi ya kimataifa, Colgate inahusika na hulipa malipo ya kila mwaka kwa mashirika kadhaa ya biashara na viwanda. Ili kuhakikisha kwamba mashirika ya kibiashara hayatumii sehemu yoyote ya malipo ya Colgate kwa michango ya kisiasa, Afisa Mkuu wa Maadili na Mwafaka wa Colgate hutuma kumbusho kila mwaka wa sera yetu kwa mashirika yote ya kibiashara ya Marekani ambako Colgate ni mwanachama anayelipa na uhitaji mashirika yote ya kibiashara ambayo hupokea kiwango fulani cha fedha za Colgate kuhusika katika mchakato wa uhakikishaji wa kila mwaka. Ili kujifunza zaidi, tafadhali rejelea Sera yetu ya Michango ya Kisiasa, ambayo inaweza kupatikana katika sehemu ya "Kampuni Yetu" ya colgatepalmolive.com.

# UHUSIANO WETU NA JAMII



*Kampuni inajitahidi kuwa mjumbe anayechangia katika jamii ya ulimwengu.*

Hapa Colgate, tunatumia ujuzi wetu katika nyanja za afya ya mdomo, kujitunza kibinafsi, kutunza nyumba na lishe ya wanyama kukuza afya na maslahi katika jamii duniani kote, na kuunga mkono mashirika ya ufadhili ambayo yana malengo kama yetu. Sisi ni raia wa kila eneo ambalo tunafanya kazi na tunashughulikia matatizo muhimu ya kiafya ikiwa ni pamoja na ukosefu wa maji safi, upatikanaji wa huduma za afya ya mdomo mdomo na ueneaji wa maradhi yanayoweza kuzuiwa.

## TUNAHUSIKA KATIKA KUCHANGIA NA KUJITOLEA KATIKA JAMII

Kupitia dunia nzima, ni lengo letu kuhusika katika miradi ya kuendeleza ukuzaji na maslahi ya watu wa jamii. Miradi kama hii inajumuisha kuhusika kwa michango ya ufadhili, na kuchukua jukumu kwa kuwasaidia maskini, majeruhi na wasiokuwa na makaazi kukiwa na janga nchini. Tunazingatia sana vijana, haswa elimu ya vijana. Colgate inaamini kuwa uwekezaji unaowekwa kwa watoto utatusaidia wote kwa siku zijazo za kesho. Hii ndio sababu Kampuni inadhamini mipango ya kusoma, ubunifu wa ushauri, mashindano ya riadha na shughuli zingine za vijana duniani kote. Juhudi hizi hukuza moyo wa kushindana na mafanikio kwenye vijana.

Kampuni pia inahimiza watu wake kuhusika kwa wakati wao wenyewe katika shughuli za mtaani za kusaidiana.

Mpango wetu wa Bright Smile Bright Future huwezesha Colgate kuathiri kwa kiwango kikubwa katika jamii tunazoishi na kufanya kazi.

**SWALI:**

Je, ninaweza kutoa muda wangu ili kufanya kazi katika kampeni ya kisiasa?

**JIBU:**

**Ndiyo.** Hata hivyo, ni muhimu kwamba shughuli zako za kisiasa zibakie kando na mahali pa kazi. Kampuni haitoi michango yoyote ya kisiasa na hakuna rasilimali zilizotolewa za Kampuni (ikiwa ni pamoja na saa za kufanya kazi au jina la Kampuni) zinazostahili kutumiwa katika shughuli hizi za kibinafsi.

## TUNASHIRIKIANA NA SERIKALI KUHUSU MATATIZO YANAYOATHIRI BIASHARA YETU

Kampuni yetu huendesha biashara katika nchi na maeneo zadi ya 200. Ni sera yetu kufanya kazi kwa ushirikiano na serikali ya mitaa na serikali ya nchi. Wakati mwingi, maswala yanayoathiri shughuli zetu yanaweza kutokea. Baada ya kuzingatia kwa makini, Kampuni inaweza kutoa maoni na mapendekezo kwa serikali kuhusu matatizo fulani ili kuunga mkono malengo na mahitaji yetu ya kibiashara. Hata hivyo, hii haistahili kufanyika kamwe bila kushauriana kwanza na meneja wako na Shirika Kuu la Kisheria.

## TUNAPINGA TABIA ZA AJIRA ZOZOTE ZA KUDHULUMU NA ZISIZO ZA UTU

Colgate inapinga ajira ya watoto, kuwatumia vibaya wanadamu na aina nyingine zote za kudhulumu wafanyakazi. Pia, ni sera ya Colgate kutofanya kazi na mgavi au mwanakandarasi yeyote anayejulikana kuwa na tabia za ajira zisizo za utu, ikiwa ni pamoja na kuwadhulumu wafanyakazi, kuwaadhibu kimwili, kuwatusi, kuwafanyisha kazi kwa kuwalazimisha au aina yoyote ya unyayasaji. Colgate haikubali ukiukaji wa sheria za wafanyakazi na ikiwa ukiukaji wowote utajulikana na Kampuni, huenda ukazingatiwa kuwa msingi wa kusitisha uhusiano wa kibiashara.

## TUNAONYESHA KUJITOLEA KWETU KWA HAKI ZA BINADAMU DUNIANI KOTE

Colgate imejitolea kwa muda mrefu kulinda haki za binadamu na haki za wafanyakazi duniani kote na huunga mkono Maamuzi ya Pamoja ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu. Colgate ilikuwa pia mmoja wa wanachama waanzilishi wa Kanuni Kuu za Sullivan. Hadi mwisho, Colgate inashughulika na kutafuta kufanya kazi na washirika wanokuza viwango vifuatavyo:

- nafasi sawa kwa waajiriwa wote katika viwango vyote bila kujali mbari, rangi, dini, jinsia, utambulisho wa jinsia, asili ya kitaifa, jamii, umri, uelekeo wa kimapenzi, ulemavu, hali ya ndoa, hali ya kuwa askari mstaafu au hali yoyote nyingine inayolindwa na sheria;
- mahali salama pa kazi ambapo panakuza maslahi na kulinda mazingira;
- malipo yanayowawezesha wafanyakazi angalau kukidhi mahitaji yao ya kimsingi, na nafasi kwa wafanyakazi kuboresha ujuzi na uwezo wao; na
- kuheshimu uhuru wa wafanyakazi wa kukutana na kutambuliwa kwa haki zote za kisheria ili kupanga na kujadiliana kwa pamoja.



# UHUSIANO WETU NA MAZINGIRA

*Mazingira safi na salama ni muhimu kwa Colgate, sio tu kwa sababu ni jambo mwafaka la kufanya, lakini kwa sababu pia ni hatua nzuri ya kibiashara. Tumejitolea kutimiza jukumu letu ili kuhifadhi rasilimali za Dunia na kudumisha maslahi ya sayari yetu kwa vizazi vijazo.*

## TUMEJITOLEA KWA UENDELEZAJI NA UWAJIBIKAJI WA KIJAMII

Hapa Colgate, tunaleta lengo letu makini la uendelezaji ambalo tunatekeleza kwa kila hali ya biashara yetu. Daima Colgate imeunga mkono kanuni za uendelezaji, na maadili yetu ya msingi - Kujali, Kazi ya Pamoja duniani, Uboreshaji Unaoendelea - huongoza juhudi zetu za uendelezaji. Mtazamo wetu unaendelea kuwa juu ya Watu, Utendajikazi na Sayari.

Isitoshe, tumejitolea kutimiza lengo letu kuu la uendelezaji ili kuhakikisha kuwa biashara ya Colgate inakua kila wakati na kwa uwajibikaji na kuwafaidisha wale tunaowahudumia, pamoja na wafanyakazi wetu, washikadau wetu, watumiaji wetu, wateja wetu na wawekezaji wengine duniani tukikuza maslahi ya vizazi vijavyo.

Kwa miaka michache iliyopita, ahadi yetu ya uendelezaji na uwajibikaji wa jamii imeongezeka kwa kuwa tumejumuisha vumbuzi hizi katika shughuli zetu za biashara, Njia hii iliyojumuishwa imetia nguvu vumbuzi zetu za uendelezaji na majukumu ya kijamii na utendaji kazi wa biashara yetu, kutusaidia kuajiri na kudumisha vipaji bora, kuboresha mahusiano yetu na washikadau, na kutoa nafasi mpya za uvumbuzi. Pengine muhimu zaidi, ahadi hii imewafurahisha na kuwahusisha watu wa Colgate duniani kote.

Kwa maelezo zaidi kuhusu mpango na miradi ya uendelezaji ya Kampuni, tafadhali rejelea sehemu yetu ya "Uendelezaji: Kupatia Dunia Sababu za Kutabasamu" kwenye colgatepalmolive.com.

## TUNALINDA NA KUTUNZA SAYARI YETU

Kampuni imejitolea kutimiza jukumu lake ili kusaidia kuokoa na kuhifadhi rasilimali za Dunia. Ahadi zetu zinazohusiana na sayari zinahusisha matumizi yetu ya kawi, uchafuzi wa hewa, matumizi ya maji na utupaji taka. Kwa hivyo, ni lazima kila mtu akubaliane na barua na moyo waa sheria na kanuni zinazotumika kwa mazingira na sera za jamii zinazowakilisha.

Tunakuza mawasiliano wazi na ya umma na tunadumisha ushirikiano unaoendelea na wa maana na jamii ambazo tunafanya kazi. Tutaendelea kushiriki maelezo na watumiaji kuhusu mkakati na mipango yetu ya kimazingira na tutafanya kazi na viongozi wa kijamii na wengine wanaoshiriki ahadi yetu.

Mipango yetu inayoendelea ya kupunguza alama ya mahusiano ya mazingira itabaki kuwa sehemu muhimu ya kutoa, kupakia na usambazaji wa bidhaa zetu.

Watu wa Colgate wanaweza kupata maelezo ya ziada kwa kurejelea maelekezo ya Kampuni yaliyo kwenye "Taarifa ya Sera ya Usalama wa Kimazingira na Kikazi" ambayo yanaweza kupatikana katika Sura ya 18 ya Maelekezo ya Kanuni za Biashara ya Kampuni yaliyo kwenye ourcolgate.com.




# UHUSIANO WETU NA WASHIKADAU

*Tunajitahidi kuhudumia mahitaji ya wawekezaji wetu na kuwasaidia kujenga thamani ya uwekezaji.*

## TUNAZINGATIA UONGOZI MZURI WA KAMPUNI ILI KULINDA THAMANI YA WASHIKADAU WETU

Uongozi wa kibiashara wa sera na mipango ya Kampuni, ambayo kanuni ya maadili mema ni sehemu muhimu sana, na inatumika kama njia muhimu ya kulinda wawekezaji. Katika miaka ya hivi karibuni vigezo vingi vya kukagua na kusawadhisha vimepitisha na Baraza Kuu la Marekani (Congress), SEC, soko la hisa la NewYork, na warekebishaji na wasimamizi wengine kote ulimwenguni ili kukuza uadilifu wa biashara ambao umekuwa zoezi la Colgate kwa muda mrefu. Washikadau wetu wanahudumiwa vizuri na bodi huru, inayohusisha wakurugenzi wengi wa kujitegemea wanaosimamia masuala ya ukaguzi, malipo na uongozi. Mikataba ya Kamati na Miongozo ya uongozi inayosasishwa mara kwa mara inafafanua vizuri shughuli na majukumu ya wakurugenzi na kanuni za kikampuni za uongozi wa Kampuni.

Kwa maelezo zaidi kuhusu mpango wa kikampuni wa uongozi wa Kampuni, tafadhali angalia "Maelekezo ya Bodi kuhusu Masuala Muhimu ya Uongozi wa Kampuni" na makubaliano ya Kamati ya Ukaguzi wa Kampuni, Kamati ya Kuteua na Uongozi wa Kampuni, Kamati ya Wafanyakazi na Shirika na Kamati ya Kifedha, zote ambazo zinapatikana kwenye colgatepalmolive.com.

## TUNADUMISHA MIPANGO THABITI YA UKAGUZI ILI KUONGEZA IMANI YA WAWEKEZAJI

Kampuni imejitoela kwa ubora, uadilifu an uwazi wa ripoti za fedha. Kujitolea huku kunaonyeshwa katika sera za muda mrefu za Kampuni na utaratibu pamoja na ukaguzi wa ndani inayoangalia udhabiti wa kifedha ulimwenguni, kamati ya wakaguzi wakujitegemea, na kamati ya wakaguzi wakujitegemea ambao wanajukumu kubwa la kusimamia sehemu hizi. Ili kuongeza ufanisi wa rasilmali hizi, watu wa Colgate wanatakikana kuhusika katika mawasiliano ya ukweli na haki na ubadilishanaji huru wa habari na ukaguzi wa nje na ndani na kamati ya wakaguzi.

Kwa maelezo zaidi kuhusiana na majukumu muhimu ya wakaguzi wa ndani wa Kampuni, wakaguzi huru na Kamati ya Ukaguzi, tafadhali angalia "Mkataba wa Kamati ya Ukaguzi," ambayo yanapatikana kwenye colgatepalmolive.com.

## TUNAWAFAHAMISHA WASHIKADAU KUHUSU MAENDELEO YA KAMPUNI

Kila mwaka wenye hisa wanaitwa kuhudhuria mkutano wa kila mwaka wa Kampuni ambapo maendeleo ya Kampuni wa mwaka uliopita yanapitiwa na wenye hisa wanapewa fursa ya kuuliza maswali kwa usimamizi mkuu wa Kampuni. Katika miezi ifuatayo, washikadau wanaweza kutembelea tovuti ya Kampuni, colgatepalmolive.com.



# UWAJIBIKAJI WA MAKUBALIANO

*Kuwa na kanuni ya maadili mema iliyoandikwa haitoshi - kuzingatia viwango vya kanuni ya maadili ni wajibu wa watu wote wa Colgate, na mwenedo wetu binafsi lazima ufanane na ahadi hii ya kudumisha viwango vya juu vya kimaadili.*

## MAWASILIANO NA UFICHUZI NI MUHIMU

Kwa kukubali ajira na Colgate, kila mmoja wetu anawajibika na makubaliano na viwango vya tabia, na sheria na kanuni zote na maongozi yenye maelezo zaidi inayopatikana katika maongozi ya shughuli za biashara na katika sera zingine, utaratibu na maongozi yanayoandaliwa na Kampuni na tanzu zake, vitendaji kazi na divisheni. Meneja wanalo jukumu la kuwasilisha viwango hivi kwa wale wanaofanya kazi nao, kuhakikisha kwamba wanavielewa na kuvifuata, na kuunda mazingira ambapo watu wanaweza kujadiliana huru masuala ya uadilifu na sheria.

## TUNA KITENGO CHA AJIRA CHA KAMPUNI KUKUSAIDIA IKIWA UNAHITAJI MWONGOZO

Kanuni haiwezi kutoa majibu ya moja kwa moja kwa maswali yote. Kwa hivyo ni lazima zaidi ya yote tutegemee ujuzi wa kila mmoja wetu kufahamu yale yanayostahili ili kufuatilia viwango vya juu vya Kampuni, ikiwa ni pamoja na uamuzi wa wakati unaofaa kutafuta ushauri mwafaka. Kama una maswali kuhusu sehemu yoyote ya maudhui yaliyojadiliwa katika Kanuni au ikiwa una shaka kuhusu hatua inayofaa zaidi katika hali fulani, tafadhali tafuta ushauri kama ilivyofafanuliwa hapa chini.

## JE, NIENDE WAPI IKIWA NINAHITAJI USAIDIZI?

**MWAJIRIWA**

**SHERIA** → Wasiliana na mwanachama wa Shirika Kuu la Kisheria ukiwa na maswali yoyote ya mwafaka au ili upate ushauri au usaidizi wa kutafsiri sheria, masharti au sera za Kampuni ikiwa ni pamoja na Maelekezo ya Kanuni za Maadili Mema ya Kibiashara.

**IDARA KUU YA MAADILI NA UTEKELEZAJI** → Unahimizwa kuwasiliana na Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji kupitia Namba ya EthicsLine ili uulize maswali, upate mwongozo kuhusu jinsi Kanuni inavyotumika kwa hali fulani au "Ongea" kuhusuiana na ukiukaji unaowezekana.

**KITENGO CHA AJIRA** → Mwakilishi wako wa Kitengo cha Ajira ni mtu wa thamani sana anayeweza kukupa ushauri na mawaidha kuhusu masuala ya kimaadili.

**MENEJA WAKO** → Zungumza na meneja wako au mwanachama wa timu ya uongozi wa shirika lako ili mjadili matatizo na maswali ya kimaadili. Ikiwa hawezi kukusaidia, atakuagizia kwa mtu anayefaa. Pia, ikiwa una wasiwasi wa kuzungumza na meneja wako, unaweza kwenda kwa Kitengo cha Ajira, Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji.

| SWALI: | JIBU: |
|---|---|
| Kama meneja, ni nini ninastahili kufanya ikiwa mmoja wa wanachama wa timu yangu "Ataongea" na kuibua hoja fulani? | Kama kiongozi, unatarajiwa kuwahimiza wengine kuongea wazi na kwa uaminifu na kuibua matatizo, hata yale nyeti. Mwanachama wa timu anapoibua hoja au anapokuomba msaada, unastahili kutokuwa na upendeleo, kuwa wazi na kuchukua hatua. Mshukuru mwanachama huyo wa timu kwa kuonyesha kujitolea kwake kwa viwango vya kimaadili vya Kampuni. Pamoja na kwamba unaweza usiwe tayari kumpa mwanachama wa timu jibu la haraka, hii ni nafasi ya kuwatumia watu wengine kama vile Kitengo cha Ajira, Shirika Kuu la Kisheria au Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji ili kukusaidia katika kumpa mwanachama huyo ushauri unaofaa. |

## "TUNAONGEA" ILI KURIPOTI MATATIZO KWA WATU WANAOFAA

Ikiwa unajua, au una sababu nzuri ya kushuku, ukiukaji wa Kanuni, Miongozo ya Kanuni ya Maadili Mema au sera nyingine za kampuni, unahitajika kuripoti moja kwa moja maelezo hayo kwa meneja wako, Kitengo cha Ajira, Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji, au Shirika Kuu la Kisheria. La sivyo, unastahili kujihisi huru kuripoti kwa ngazi za juu za usimamizi bila woga wa kulipiziwa kisasi.

## NINAWEZAJE KUWA NA UHAKIKA KWAMBA HAKUNA HATUA YOYOTE MBAYA ITACHUKULIWA DHIDI YANGU?

Unaweza kuwasiliana na Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji kwa kutumia Namba ya EthicsLine ya Colgate-Palmolive.

Maelezo yote yaliyotolewa kupitia Namba ya EthicsLine hukaguliwa na, ikiwa yanahusiana na Kanuni, suala hilo huchunguzwa kisawasawa na Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji na/au Shirika Kuu la Kisheria. Ni muhimu kwamba watu wanaoripoti wasifanye uchunguzi wao binafsi kwani unaweza kusababisha maswala magumu ya kisheria. Kuchukua hatua mwenyewe kunaweza kuvuruga uaminifu wa uchunguzi na kuathiri kwa kiasi kikubwa wote wewe na Colgate.

Ripoti zinaweza kutolewa kwa siri iwapo sheria za nchi husika zinaruhusu. Lakini, tunakuhimiza ujitambulishe wakati unapiga simu ili utusaidie kuwezesha uchunguzi na ufuatiliaji. Kuna sheria katika nchi nyingine ambazo zinakataa aina ya habari unazoweza kuripoti kupitia kwa nambari ya haraka. Ikiwa sheria hizi zinatumika katika hali yako, mwakilishi wa Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji atakuelekeza kwa mtu katika kitengo chako cha biashara ambaye anaweza kukusaidia na swali au suala lako.

Hata hivyo, kumbuka kwamba ikiwa ungetaka kujitambulisha, Kampuni itachukua hatua zote zinazofaa kulinda ufaragha wa utambulisho wako na maelezo yako yaliyowasilishwa, na itafichua maelezo kwa msingi wa kuhitaji kujua pekee wakati ufichuzi:

- Unafaa ili kutekeleza uchunguzi mwafaka na kuchukua hatua inayofaa; au
- Ikihitajika na sheria husika.

Ripoti au malalamiko yanaweza kuwa na data ya kibinafsi. Kwa lengo la uchunguzi wa ukiukaji au ukiukaji unaoshukiwa, huenda ikawa muhimu, kulingana na sheria, kuhamisha data ya kibinafsi iliyokusanywa katika nchi moja hadi nchi nyingine, ikiwa ni pamoja na Marekani. Katika hali kama hizo, data ya kibinafsi inayotumiwa na wafanyakazi na mashirika ya Colgate ambayo yanahusika katika shughuli za Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji kuchunguza ripoti hiyo, lakini kwa muda mfupi tu kama itakavyotakikana kwa lengo hili (na baadaye data hiyo ya kibinafsi itaharibiwa ama itawekwa kama inavyotakikana na sera ya Kampuni au sheria).

## NAMBARI YA ETHICSLINE

**ethics@colpal.com**

**(800) 778-6080**
**(simu ya bure nchini Marekani, Kanada na Puetoriko)**
**1-(212) 310-2330**
**(laini ya kupigiwa tena kutoka maeneo mengine yote)**

**Global Ethics & Compliance**
**Colgate-Palmolive Company**
**300 Park Ave, 5th Floor**
**New York, NY 10022**

**Zana ya Wavuti**

**Faksi**
**(212) 310-3745**


**SWALI:**

Nimesikia kwamba maoni yangu yanaleta utofauti lakini hivi karibuni nimemwendea meneja wangu "Kuongea" kuhusu suala muhimu, lakini hakuna chochote kilichofanyika. Je, ninastahili kufanya nini sasa?

**JIBU:**

Wote tunawajibika kuhakikisha kwamba Kampuni yetu inadumisha utamaduni wa uadilifu na viwango vya juu vya kimaadili. Ikiwa huamini kwamba hatua inayofaa imechukuliwa ili kushughulikia hofu zako, una njia nyingine kadhaa za ziada. Usiogope kuelekeza suala hilo kwa ngazi za juu zaidi na "Uongee" na usimamizi wa ngazi ya juu inayofuata, Kitengo cha Ajira, Shirika Kuu la Kisheria, Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji. Kampuni inashukuru kwa juhudi zako za kuelekeza suala hili kwa ngazi za juu.

## JE, NI NINI HUFANYIKA BAADA YA KUWASILIANA NA NAMBA YA ETHICSLINE?



## MCHAKATO WA UCHUNGUZI WA COLGATE

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| GE&C hupangia Mchunguzi ambaye hausiani na kitengo cha biashara ambacho ripoti ilitolewa. | Mchunguzi ataendesha uchunguzi. | Mchunguzi hutoa matokeo. | Idara Kuu ya Maadili na Utekelezaji itapitia matokeo na kutoa mapendekezo ya hatua kwa utekelezaji. | Mwisho wa uchunguzi, mtu aliyeripoti suala hilo atapewa maoni (ikiwa maelezo ya mawasiliano yalitolewa). |

## HATUA ZA KINIDHAMU ZINAWEZA KUCHUKULIWA

Kampuni ina sera ya "kutokubali kabisa" tabia yoyote ambayo inakiuka Kanuni au Mwongozo wa Desturi za Biashara. Hii inamaanisha kwamba wakati tukio la ukiukaji limethibitishwa, hatua inayofaa itakayochukuliwa italingana na hali na kiasi cha ukiukaji. Hakuna mtu au meneja katika Kampuni mwenye ruhusa kuhusika katika tabia isiyozingatia Kanuni hii, au kuidhinisha, kuelekeza, au kukubali tabia yoyote kama hiyo na mtu mwingine. Vivyo hivyo, Kampuni inakusudia kuzuia tukio la tabia isiyolingana na Kanuni au Mwongozo wa Desturi za Biashara na kukomesha tabia yoyote kama hiyo ambayo inaweza kutokea punde tu inapowezekana baada ya utambuaji wake. Watu wa Colgate wanaokiuka Kanuni au Mwongozo wa Desturi za Biashara huenda wakachukuliwa hatua za nidhamu, hadi kujumuisha kusitishwa, kulingana na sheria ya nchini.

## KANUNI HIZI ZINAHUSU WATU WOTE WA COLGATE NA SHUGHULI ZA KAMPUNI

Kuzingatia Kanuni ya Maadili Mema na Mwongozo wa Kanuni za Biashara kutasimamiwa na Idara Kuu ya Maadili na Mwafaka. Idara huripoti kwa Afisa Mkuu Mtendaji/Mwenyekiti wa Bodi na Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi wa Bodi la Wakurugenzi wa Colgate juu ya kuanzishwa, kutekelezwa na kuhakikisha kufuatwa kwa Kanuni ya Maadili Mema na mipango husika.

Maelezo yaliyoripotiwa kwa Idara Kuu ya Maadili na Mwafaka au kupitia njia nyingine ni, kama inavyofaa, huwasilishwa kwa msingi wa usiri kwa Kamati ya Ukaguzi.

Kanuni inatumika kwa kila mtu anayefanya kazi na Kampuni ya Colgate-Palmolive na kampuni zake tanzu, ikiwa ni pamoja na maafisa, na hutumika pia kwa wakurugenzi na mawakala wa Kampuni kulingana na sheria husika. Nakala za Kanuni zinapatikana mtandaoni kwenye tovuti yetu ya ndani ya intraneti na pia tovuti yetu ya nje na zinastahili kutolewa kwa wahusika wote wengine waliodhinishwa kutenda kwa niaba ya kampuni. Watu wa Colgate duniani kote wanaonyesha kujitolea kwao kwa makubaliano na viwango vya uadilifu vya Kampuni kwa kuhusika katika mafunzo na vyeti vya Kanuni ya Maadili Mema kila mwaka.

COLGATE-PALMOLIVE COMPANY

300 Park Avenue
New York, NY 10022
212-310-2000
www.colgatepalmolive.com